

VUANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Tatu

Kitabu cha Nne



MUNGU WETU MKUU

VUANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Tatu

Kitabu cha Nne

Africa Coordinated Curriculum for
Bible Study

J3 - 4P

Published and printed by
Baptist Publications House
Box 30370 Nairobi


VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Tatu

Kitabu cha Nne

Y A L I Y O M O

<u>Sura</u>	<u>Ukurasa</u>
Ujumbe kwa Mwanafunzi.....	5
1. Njia ya Mungu.....	7
2. Utunzi wa Mungu.....	13
3. Msamaha wa Mungu.....	18
4. Wema wa Mungu.....	24
5. Tumsifu Mungu wetu Mkuu.....	29
6. Ujumbe wa Mungu.....	36
7. Utii kwa Mungu.....	44
8. Hukumu ya Mungu.....	53
9. Masharti ya Mungu.....	60
10. Mungu Amwita Nabii.....	68
11. Masihi Atabiriwa.....	75
12. Kristo Amezaliwa.....	81
13. Tunu zetu kwa Yesu.....	88



UJUMBE KWA MWANAFUNZI

Mungu anatwambia katika Neno lake kwamba inatupasa kukua katika neema na katika kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. (Soma 2 Petro 3:18.) Wakati unapojifunza masomo haya tunakuomba kwamba utakua katika kumjua Mungu na Mwanawe Yesu ambaye ni Mwokozi wa ulimwengu.

Pili, tutajifunza juu ya manabii. Je! manabii walikuwa watu gani? Walikuwa watu walioitwa na Mungu kuhubiri ujumbe wake. Manabii wengi wa Kiebrania waliishi baada ya Daudi na Sulemani kufa. Wakati Sulemani alipokufa, ufalme wa Waebrania uligawanyika katika falme mbili, Yuda na Israeli.

Falme hizi mbili zilikuwa na wafalme wachanga wema na wengi walikuwa wabaya. Wengi walikuwa wakatili na wadhalimu. Hawakujali watu wao. Hawakumwabudu Mungu.

Mungu aliwavumilia sana watoto hawa wake ambao hawakumtii. Aliwapenda na aliwapa nafasi nyingi sana kumrudia. Aliwatumia manabii kila mara kuwahubiria. Manabii hao waliwaonya juu ya mambo ambayo yangewapata kama nchi yao ingeendelea katika hali hiyo ya dhambi.

Iliwapasa manabii kuwa mashujaa. Haikuwa kazi rahisi kuwaambia wafalme kwamba Mungu angewaadhibu. Wakati watu hao walipowasikiliza manabii na kutii, Mungu aliibariki sana nchi yao.

Manabii wengine waliuawa. Wengine walifungwa gereza. Miji mingi ya

Waisraeli iliharibiwa na watu walikama-twa mateka.

Ingawa manabii waliwahubiria Waisraeli, ujumbe wao bado ni muhimu sana hata kwetu sisi leo. Mungu bado anataka uaminifu wetu. Anatuadhibu wakati tunapokataa kumtii. Lakini anawabariki sana wale wanaomcha na kumfuata.

Tatu, tutajifunza juu ya furaha ya Krismasi. Sababu ya kuwa na furaha wakati wa Krismasi ni kwamba Wakristo hushehekea kuzaliwa kwa Mfalme wa wafalme. Tunaweza kuwa na furaha hiyo mioyoni mwetu ikiwa Mfalme wa wafalme, Bwana wetu Yesu Kristo, anaishi ndani ya mioyo yetu.

Watu wengi hufikiria kupokea tu wakati wa Krismasi. Hebu sisi Wakristo tufikirie kutoa, kutoa upendo wetu kwa watu hawa wanaotazamia tu kupokea. Waambie habari za kipawa kikuu cha Mungu kwetu ambaye ni Yesu Kristo.

Toa namna ya vipawa ambavyo Yesu alitoa wakati huu wa Krismasi. Wewe huwezi kumponya mgonjwa, lakini unaweza kumtembelea na kumfanya kuwa na furaha. Unaweza kutoa usaidizi wako kwa watu wenyewe shughuli nyingi. Unaweza pia kufanya urafiki na watu walio katika hali ya upweke. Wakumbuke wazazi, ndugu, na dada zako katika njia maalum.

Mwenyezi Mungu akubariki na kuufanya wakati huu wa Krismasi kuwa wa maana na furaha katika Mwokozi wetu Yesu Kristo.

NJIA YA MUNGU


MASOMO YA BIBLIA: Zaburi 1

Je! unajua kwamba Biblia inasema watu wengine ni kama miti? Unaweza kufikiria njia ambayo watu wanaweza kuwa kama miti? Watu hawafanani na miti. Tunaweza kufikiria njia ambazo watu wanato-fautiana na miti. Wakati tunapojifunza andiko la somo hili, tunatambua namna ya mtu ambaye ni kama mti.

Andiko la somo hili ni Zaburi 1. Katika andiko hili tunasimuliwa habari za watu wawili mbalimbali. Mtu wa kwanza ni wa haki. Kifungu cha kwanza kinatwambia mambo ambayo hafanyi. Hafuati masha- uri ya wasio haki. Haendi mahali ambapo wenye dhambi wanakusanyika kutenda maba- ya. Haketi pamoja na watu wenye mizaha wanaochea vitu vya Mungu. Hafanyi ura- fiki na watu kama hao.

Kifungu cha pili kinatwambia mambo ambayo mtu wa haki hufanya. Hufurahi kufanya mambo yote ambayo Mungu anamtaka kufanya. Hufikiria Neno la Mungu mchana na usiku. Hufikiria njia hasa za kumfu- ata Mungu.

Somo hili linaitwa "Njia ya Mungu". Mtu wa haki hutafuta njia ya Mungu daima. Mungu hutufundisha njia yake katika Neno lake takatifu. Mtu huyu wa haki, anaye- mpenda Mungu na Neno lake, ni kama mti uliopandwa kando ya mto. Kila mwaka mti huo huzaa matunda katika wakati unaofaa.



Majani yake
hayakauki
kwa sababu
mizizi yake
ina maji
kila mara.
Mtu wa haki
huzaa matu-
nda maisha-
ni mwake.
Tunafundi-
shwa juu ya
matunda
haya katika

Wagalatia 5:22-23. Matunda ya Mkristo ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, na kiasi. Je! una matunda haya maishani mwako? Ikiwa unatembea katika njia ya Mungu, una matunda haya maishani mwako.

Yesu alizungumza juu ya watu wa namna mbili, mwenye akili na mpumbavu. Yesu alisimulia hadithi ifuatayo katika Mathayo 7:24-27: "Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafaninishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafaninishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa."



Tunasimulia habari za mtu asiye haki katika Zaburi 1:4. Yeye ni kama makapi yapeperushwayo na upepo. Hana thamani. Wakati wa hukumu utakapofika, hatahesabiwa haki. Hatapatikana miongoni mwa

watu wanaopenda na kufuata njia ya Mungu. Mungu anajua watu wanaotembea katika njia yake. Njia ya wasio haki itapotea.

Je! utakuwa kama mtu wa haki anayefurahi kwa sababu anapenda Neno la Mungu na anafanya jambo linalosema? Je! utakuwa kama mtu mwenye akili anayejenga misha yake juu ya msingi wa Neno la Mungu?

Au utakuwa kama mtu asiye haki anayepeperushwa na upepo kama makapi kwa sababu hatembelei katika njia ya Mungu? Je! utakuwa kama mtu mpumbavu ambaye hasikilizi Neno la Mungu na anayekataa kutenda kama Neno hilo linavyosema?

Katika Mithali 16:25 tunasoma, "Iko njia ione kanayo kuwa sawa machoni pa mtu; lakini mwisho wake ni njia za mauti." Ni jambo la kuhuzunisha sana kuwafikiria watu wengi wanaofikiri kwamba wako katika njia ya haki, lakini wako katika njia ya mauti.

MUNGU WETU MKUU

Yesu alizungumza juu ya njia mbili katika Mathayo 7:13, 14. Alisema kwamba njia iendayo upotevuni ni pana. Watu wengi wako katika njia hiyo pana. Njia iendayo uzimani ni nyembamba. Watu wacha-che ndio wanaofuata njia hii.

Ikiwa unafuata njia ya Mungu, uko katika njia hiyo nyembamba iongozayo uzimani na furahani. Ikiwa hufuati njia ya Mungu, uko katika njia ile pana iongozayo upotevuni na uangamizi wa milele.

Fikiria kwa makini sana juu ya maisha yako. Ikiwa bado hujamwomba Yesu kuingia moyoni mwako, je! utafanya hivyo leo? Ukifanya hivyo, utakuwa kama mtu yule wa haki na mwingine yule mwenye akili ambao umekwisha kujifunza habari zako leo. Utakuwa kama mti uliopandwa kando ya mto ambao huzaa matunda kila siku na ambao haunyauki. Utajenga maisha yako juu ya msingi wa Neno la Mungu. Utafuata njia ile nyembamba iongozayo uzimani!



Nyumba iliyojengwa juu ya mwamba.



Nyumba iliyojengwa juu ya mchanga.

KAZI YA KUFANYA:

Hapa kuna sentensi zinazoeleza habari za mtu wa haki na mtu asiye wa haki. Andika namba ya sentensi katika mstari ulio chini ya jina la mtu ambaye sentensi hiyo inaeleza habari zake.

1. Hafuati mashauri ya watu wasio haki.
2. Yeye ni kama makapi yapeperushwayo na upepo.
3. Siku ya hukumu itakapofika, hata-simama pamoja na watu wa haki.
4. Hufikiria Neno la Mungu mchana na usiku.

MTU WA HAKI

MTU ASIYE WA HAKI

Katika mistari hiyo hapo chini, andika matunda ya Mkristo yaliyo katika Wagalatia 5:22-23.

_____	_____	_____
_____	_____	_____
_____	_____	_____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Kwa kuwa Bwana anaijua njia ya wenye haki, bali njia ya wasio haki itapotea." Zaburi 1:6

MUNGU WETU MKUU

Mungu anaona kila kitu tunachofanya. Anajua mawazo ya roho zetu. Anatumza maisha ya wale wanaompenda na wanaotembea katika njia yake. Lakini anasema wazi kwamba mtu asiye haki anayemkataa pamoja na njia yake, atapotea.

MANENO YA KUJIFUNZA:

mizaha.....dhihaka, ubishi, mchezo.
makapi.....wishwa.
haunyauki.....haukauki.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Zaburi 1

Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; Wala hokusimama katika njia ya wakosaji; wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. (2) Bali sheria ya BWANA ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku. (3) Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji; uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa. (4) Sivyo walivyo wasio haki; Hao ni kama makapi yapeperushwayo na upepo. (5) Kwa hiyo wasio haki hawatasi mama hukumuni, wala wakosaji katika kusaniko la wenye haki. (6) Kwa kuwa BWANA anajua njia ya wenye haki, Bali njia ya wasio haki itapotea.

UTUNZI WA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Zaburi 23

Wanafunzi ambao wamekwisha kuchunga ng'ombe, mbuzi au kondoo; za baba zao, wanaelewa hadithi hii yetu vyema sana. Kazi ya kuchunga mifugo ni kazi muhimu sana.

Andiko la somo hili ni Zaburi 23. Daudi ndiye aliyeandika Zaburi hii. Kati-ka Zaburi 23:1 alisema, "Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu." Wakati Daudi alipokuwa kijana, alikuwa mchungaji. Alijua jinsi ilivyokuwa muhimu kwake kuchunga kondoo za baba yake. Ali-kuwa mwaminifu na shujaa sana katika kazi yake.



Ilikuwa kazi ya Daudi kutafuta mahali penye majani mabichi kuwalisha kondoo zake. Aliwaongoza hadi vijito kunywa maji. Katika nchi ile kavu ambayo

MUNGU WETU MKUU

Daudi alikaa, haikuwa rahisi kupata maji. Kondoo huenda tu mahali wanapoongozwa. Bila mchungaji mwaminifu, kondoo hao waweza kupotea au kuuawa na wanyama wa mwitu.

Daudi hakuogopa. Siku moja aliua simba aliyekuwa akijaribu kukimbia na kondoo mmoja. Wakati mwingine alimwua dubu. Kitendo hiki kinaonyesha jinsi alivyokuwa shujaa. Alikuwa na imani kuu katika Mungu. Alijua kwamba Mungu alikuwapo pamoja naye sikuzote. Wakati alipoandika Zaburi hii, alisema Mungu alimlinda kama yeye alivyowalinda kondoo zao wakati alipokuwa mchungaji.

Daudi alijua kwamba kwa sababu Mungu alikuwa akimtunza, hakupungukiwa na kitu cho chote. Mungu alimpa mahitaji yake yote. Hata wakati alipokuwa hatari ni Mungu alimtunza.

Daudi alijifunza kumwamini Mungu wakati alipokuwa kijana mchungaji. Katika kukua kwake, aliendelea kumwamini Mungu. Imani yake katika Mungu ilimwezesha kumwua Goliathi aliyekuwa jitu.

Daudi alipokuwa mtu mzima alijiunga na kazi ya jeshi. Aliandika katika Zaburi 27:3, "Jeshi lijapojipanga kupigana nami, moyo wangu hautaogopa. Vitu vijaponitokea, hata hapo nitatumaini."

Yesu alisema katika Agano Jipya kwamba yeye ni mchungaji mwema. Alisema katika Yohana 10:11, "Mimi ndimi mchungaji-

ji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo."

Yesu alisema katika Yohana 10:14, "Mimi ndimi mchungaji mwema; nao walio wangu nawajua; nao walio wangu wanjua mimi."



Tunasoma katika Yohana 10:27, 28, "Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wani-fuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu."

Basi, unaweza kuona kwamba Yesu anasema yeye ni mchungaji wetu. Ni jambo jema na la ajabu kujua kwamba anatutunza katika njia hiyo.

Anamtunza kila mmoja wetu. Hata kama wewe ni mtu wa aina gani, Mungu anakupe-nda. Anakujua. Anatazama moyo wako. Ana-ona dhambi iliyo katika maisha yako. Ana-kwambia utubu dhambi zako kwake. Atakusa-mehe dhambi hizo. Atakuwa mchungaji wako. Atakutunza sikuzote. Anasema kwamba haku-na kitu kinachoweza kukupokonya katika mkono wake.

MUNGU WETU MKUU

Je! unaweza kufikiria njia ngapi ambazo Mungu anakutunza? Je! umekwisha kuhesabu baraka zake kwako? Tumia dakika chache kufanya hivyo sasa. Kisha kuwa na wakati wa maombi kumshukuru Mungu kwa utunzi wake kwa kila mmoja wetu.

KAZI YA KUFANYA:

Andika mambo manne ambayo mchungaji mwema huwafanyia kondoo zake katika mistari hiyo hapo chini.

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____

Jaza nafasi zilizoachwa kwa maneno yanayofaa:

"_____ wangu waisikia _____
yangu; nami nawajua, nao wanifuata.
Nami nawapa _____ wa _____;
wala hawatapotea kamwe; wala hakuna
mtu atakayewapokonya katika _____
wangu." (Yohana 10:27,28)

Andika njia nyingine ambazo Mungu hukutunza katika mistari hiyo hapo chini. Andika njia nyingi kama unavyoweza kufikiria.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Bwana ndiye mchungaji wangu, sita-
pungukiwa na kitu." Zaburi 23:1

Kwa sababu Bwana ndiye mchungaji wako, atakutunza. Atakupa kila kitu una-chohitaji. Je! unaamini kweli kwamba atakufanyia hivyo? Daudi alisema kwamba hakuogopa hata kifo kwa sababu Mungu alikuwapo pamoja naye. Endelea kukua katika ufahamu wako juu ya Mungu mpaka uweze kumwamini yeye kwa kila kitu una-chohitaji.

MANENO YA KUJIFUNZA:

dubu.....namna moja ya mnyama wa
mwituni.
pokonya.....kunyang'anya, kutwaa kwa
nguvu, kuiba kwa nguvu,
kukwepua.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Zaburi 23

BWANA ndiye mchungaji wangu, sitapu-
ngukiwa na kitu. (2) Katika malisho ya
majani mabichi hunilaza, Kando ya maji
ya utulivu huniongoza. (3) Hunihuisha
nafsi yangu; na kuniongoza katika njia
za haki kwa ajili ya jina lake. (4)
Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli
wa mauti, Sitaogopa mabaya; Kwa maana
Wewe upo pamoja nami, Gongo lako na
fimbo yako vyanifariji. (5) Waandaa meza
mbele yangu, Machoni pa watesi wangu.
Umenipaka mafuta kichwani pangu, na kiko-
mbe changu kinafurika. (6) Hakika wema
na fadhili zitanifuata sikuzote za mai-
sha yangu; Nami nitakaa nyumbani mwa
BWANA milele.

MSAMAHA WA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Zaburi 51:1-4, 10-14;
Mathayo 6:12-15



Je! ume-
mwomba mtu
fulani uliye-
mkosea kukupa
msamaha naye
akakataa ku-
kusamehe?
Ikiwa jambo
hili liliku-
fanyikia,
bila shaka
lilikuudhi
sana. Uliomba
msamaha kwa
sababu ulijua
moyoni mwako
kwamba ulite-
nda kosa.
Kutosamehewa
kunahuzunisha
sana.

Ajabu moja tuliyojifunza juu ya
Mungu wetu mkuu ni kwamba anasamehe.
Zaburi 130:4 inasema, "Lakini kwako kuna
msamaha, ili wewe uogopewe."

Tunasoma katika Waefeso 1:7, "Katika
yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi
wetu, msamaha wa dhambi." Mungu alimtuma
Mwanawe pekee ulimwenguni. Yesu alikufa
kwa ajili ya dhambi zako. Mshahara wa
dhambi ni mauti kwa hivyo inatupasa kufa

kwa dhambi zetu. Lakini Yesu alikufa badala yetu. Tunapomwamini na tunapotubu dhambi zetu, Mungu hutusamehe.

Andiko la somo hili ni Zaburi 51. Katika Zaburi hii Daudi alimwomba Mungu kumhurumia na kumsamehe. Alimwomba Mungu kumwosha dhambi zake. Alikuwa na hatia ya dhambi mbili kubwa sana. Anasema katika Zaburi 51:3, "Maana nimejua mimi makosa yangu, na dhambi yangu i mbele yangu daima."

Daudi alitwaa mke wa mtu mwingine. Alimfanya mume wa mke huyo kuuawa vitani. Kwa hivyo, Daudi alikuwa na hatia ya uzi-nzi na uuaji. Alipoteza amani na furaha yake. Alifikiria tu dhambi yake kuu ali-yomtenda Mungu.

Daudi aliomba, "Ee Mungu, uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu. Usinitenge na uso wako, wala roho yako mtakatifu usiniondolee. Unirudishie furaha ya wokovu wako...." (Zaburi 51:10-12)

Mungu alimsamehe Daudi kama anavyo-msamehe kila mmoja wetu anapotubu dhambi zake kwake. Tuna ahadi ya ajabu katika 1 Yohana 1:9 inayosema, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

Hakuna dhambi kuu zaidi isiyoweza kusamehewa. Wala hakuna dhambi ndogo zaidi isiyoweza kuungamwa. Hata tukiwa

MUNGU WETU MKUU

na dhambi za namna gani mioyoni mwetu inatupasa kuziungama mara moja. Tusipoungama hatuwezi kusamehewa. Ikiwa moyo wako hauna furaha labda ni kwa sababu kuna dhambi ambayo hujaungama kwa Mungu.

Tunasoma katika Zaburi 66:18, "Kama ningaliwaza maovu moyoni mwangu, Bwana asingesikia." Kifungu hiki kinaeleza wazi kwamba tukiwa na dhambi mioyoni mwetu, Mungu hatatusikia. Ni lazima tuungame dhambi zetu kila siku. Kisha tunaweza kuwa na ushirika wa ajabu pamoja na Baba yetu aliye mbinguni.

Swali la kwanza katika somo hili liliuliza, "Je! umemwomba mtu fulani uliyemkosea kukupa msamaha naye akakataa kukusamehe?" Sasa swali la pili linauliza, "Je! umekataa kumsamehe mtu fulani aliyekuomba msamaha?" Sikiliza maneno haya ambayo Yesu alisema: "Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu." (Mathayo 6:14,15) Yesu anasema kwamba ukikataa kuwasamehe watu wengine, Mungu hatakusamehe wewe pia.

Siku moja Petro alimjia Yesu, akamwuliza, "...Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? hata mara saba? Yesu akamwambia, sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini." (Mathayo 18:21b-22) Yesu alikuwa na maana kwamba ni lazima tumsamehe mtu ye yote anayetuomba msamaha kila wakati

anapotuomba. Wakati mwingine ni vigumu sana kusamehe, lakini Mungu anatwamuru kusamehe kwa hivyo atatusaidia.

Waefeso 4:32 ni kifungu kingine juu ya msamaha. Labda unakijua kwa moyo. Kinasema, "Sema, Iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi."

Mungu hutusamehe kwa sababu anatupe-nda sana. Siku hii ya leo ujaribu kukaa peke yako kwa muda fulani. Ungama dhambi zako kwa Mungu na umwombe kukusamehe. Yeye ni mwaminifu kwa ahadi yake kukusamehe. Utakuwa na furaha kuu moyoni mwako.

KAZI YA KUFANYA:

Hapa kuna vifungu vya somo hili letu la leo. Andika maneno yanayofaa katika nafasi zilizoachwa.

"Lakini kwako kuna _____, ili wewe uogopewe." (Zaburi 130:4)

"Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao _____ wetu, _____ ya dhambi, sawasawa na wingi wa _____ yake." (Waefeso 1:7)

"Maana nimejua mimi _____ yangu, na _____ yangi i mbele yangu daima." (Zaburi 51:3)

MUNGU WETU MKUU

"Kwa maana mkiwasamehe watu _____
yao, Baba yenu wa mbinguni _____
ninyi. Bali _____ watu makosa
yao, wala Baba yenu _____ ninyi
makosa yenu." (Mathayo 6:14, 15)

Andika maneno sawa katika mistari
ili kukamilisha sentensi zifuatazo:

1. Hakuna dhambi kubwa zaidi isiyowe-
za _____.
2. Hakuna dhambi ndogo zaidi isiyowe-
za _____.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Ee Mungu, uniumbie moyo safi, uifa-
nye upya roho iliyotulia ndani
yangu."* Zaburi 51:10

Tunapotenda dhambi, tunakuwa na
aibu mioyoni mwetu. Tunajiona kuwa wacha-
fu kindani. Tunajiona kuwa mbali sana na
Mungu. Lakini Mungu yupo karibu nasi.
Anangojea tutubu dhambi zetu kwake ili
aweze kutusamehe na kutubariki. Unapo-
mwomba Mungu kukupa moyo ulio safi, kama
Daudi alivyofanya, atakupa.

MANENO YA KUJIFUNZA:

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Zaburi 51:1-4


Ee Mungu, unirehemu, Sawasawa na fadhili zako. Kiasi cha wingi wa rehema zako, Uyafute makosa yangu. (2) Unioshe kabisa na uovu wangu, Unitakase dhambi zangu. (3) Maana nimejua mimi makosa yangu, Na dhambi yangu i mbele yangu daima. (4) Nimekutenda dhambi Wewe peke yako, Na kufanya maovu mbele za macho yako. Wewe ujulikane kuwa una haki unenapo, Na kuwa safi utoapo hukumu.

Mathayo 6:12-15

Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. (13) Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. [Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.] (14) Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. (15) Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.

WEMA WA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Zaburi 100



Je! kuna mtu ye yote ambaye amepima mbingu? Je! milima imepata kupimwa? Bahari je? Labda maswali hayo yanaweza kufikiriwa kuwa ya kipumbavu kwa sababu vitu hivyo haviwezi kupimwa. Lakini Mungu wetu mkuu aliumba ulimwengu huu mzuri. Aliumba kwa ajili yetu sisi kuwa na mahali pa kukaa. Uzuri wa ulimwengu huu unaonyesha wema na upendo wa Mungu. Daudi alisema, "Jinsi zilivyo nyingi fadhili zako ulizowawekea wakuchao; ulizowate-ndea wakukimbiliao...." (Zaburi 31:19)

Siku hii ya leo uko hapa kwa sababu ya wema wa Mungu. Unapumwua. Unaweza kuona. Unaweza kusikia. Unaweza kusema. Unaweza kutembea. Je! umekwisha kumshukuru Mungu kwa vitu hivyo? Hizi ni baadhi ya baraka ulizo nazo kwa sababu ya wema wa Mungu.

Wema wa Mungu unaonekana katika upe-
 ndo wake kwa kila mtu. Anataka kila mtu
 aokolewe. Tunasoma katika 2 Petro 3:9,
 "Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake,
 kama wengine wanavyokudhani kukawia,
 bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu
 ye yote apotee, bali wote wafikilie
 toba." Ye yote anayemwamini Yesu hatapo-
 tea bali atakuwa na uzima wa milele.
 Mungu hataki mtu ye yote kupotea na kwe-
 nda motoni.

Wakati mwingine tunajaribu kupima
 wema wa Mungu kwa vitu alivyotupa amba-
 vyo tunaweza kuviona au kuvigusa. Lakini
 wema wa Mungu hupimwa hasa kwa vitu ana-
 vyotupa ambavyo hatuwezi kununua kwa
 pesa. Je! vipawa hivi vya Mungu ambavyo
 hatuwezi kununua kwa pesa ni nini? Bila
 shaka unaweza kutaja vingi. Tumekwisha
 kuzungumza juu ya vingine. Je! ni vipawa
 gani ambavyo tumekwisha kuzungumza juu
 yao ambavyo vinaonyesha wema wa Mungu?

Kitu kingine kinachoonyesha wema wa
 Mungu ni rehema yake kwetu. Tunatenda
 dhambi mara kwa mara. Lakini kila wakati
 tunapotubu na kuomba msamaha, Mungu hutu-
 samehe. Hachoki kutusamehe.

Ahadi za Mungu zinaonyesha wema
 wake kwetu. Anaahidi kutupa kila kitu
 tunachohitaji. (Soma Wafilipi 4:19.)
 Mungu hakuahidi kutupa kila kitu tunacho-
 taka bali ameahidi kitu tunachohitaji
 hasa. Akikupa kila kitu tunachotaka hai-
 taonyesha wema wake. Kwa sababu anatupe-
 nda sana, atatupa vitu vilivyo vyema
 kwetu.

Wema wa Mungu huonekana wakati wa taabu. Mtu ye yote unayempenda anapokufa, Mungu atakufariji. Labda utaona uchungu mwingi moyoni mwako, lakini ukimwomba Mungu kukupa amani, atafanya hivyo. Tunaona wema wa Mungu katika uaminifu wake kujibu maombi yetu.

Je! unaogopa daima? Hakika, utajibu, "ndiyo." Kila mtu huogopa wakati mwingine. Lakini Mungu hataki tuogope. Kwa sababu yeye ni mwema sana, ataondoa woga wetu na atatupa amani. Daudi alikuwa na mambo mengi ya kuogopa. Kulikuwa na maadui waliokuwa wakijaribu kumwua. Lakini alisema, "Siku ya hofu yangu nita-kutumaini Wewe; kwa msaada wa Mungu nitalisifu neno lake. Nimemtumaini Mungu, sitaogopa; mwenye mwili atanitenda nini?" (Zaburi 56:3-4)

Je! unaweza kusema maneno hayo kwa uaminifu hasa? Ikiwa huwezi, umwombe Mungu kukuondolea woga wako juu mambo yote, na atakufanyia hivyo.

Je! umekwisha kuona wema zaidi wa Mungu kwako? Mshukuru kwa mambo yote yanayoonyesha wema wake kwako. Kuwa mwaminifu katika kuonyesha shukrani yako kwake.

KAZI YA KUFANYA:

Hapo chini kuna orodha ya majina ya vitu. Chagua majina ya vitu unavyoweza kununua kwa pesa na kuyaandika chini ya maneno haya, vitu vinavyoweza kununuliwa

kwa pesa. Uandike majina ya vitu ambavyo huwezi kuvinunua kwa pesa chini ya maneno haya, Vitu ambavyo haviwezi kununuliwa kwa pesa. Unapomaliza, uchague orodha yenye majina ya vitu ambavyo ungependa kuwa navyo.

VITU VINAVYOWEZA
KUNUNULIWA KWA
PESA

VITU AMBAVYO
HAVIWEZI KUNUNU-
LIWA KWA PESA

(Miguu, mkate, maziwa, mikono, chai, matunda, afya, mahindi, nyama, nguvu, macho, motakaa, furaha, blanketi, tandiko, amani, msamaha, nguo, uzima wa milele.)

Je! unaweza kuona sasa kwamba tuna-weza kupata vitu hivi vya ajabu ambavyo hatuwezi kununua kwa pesa kwa sababu ya wema wa Mungu?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Kwa kuwa Bwana ndiye mwema; rehema zake ni za milele; na uaminifu wake vizazi na vizazi."

Zaburi 100:5

MUNGU WETU MKUU

Ni jambo jema na la ajabu kujua kwamba Mungu anatupenda sikuzote. Yu mwema sikuzote. Amekuwa mwaminifu sikuzote. Wakati tunaposoma Biblia, tunaona uaminifu wake tangu mwanzo hadi mwisho. Yeye ni kama jana leo na hata milele.

MANENO YA KUJIFUNZA:

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Zaburi 100

Mfanyieni BWANA shangwe, dunia yote; (2) Mtumikieni BWANA kwa furaha; Njoni mbele zake kwa kuimba; (3) Jueni kwamba BWANA ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; Tu watu wake, na kondoo wa malisho yake. (4) Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; Nyuani mwake kwa kusifu; Mshukuruni, lihimidini jina lake; (5) Kwa kuwa BWANA ndiye mwenye; Rehema zake ni za milele; Na uaminifu wake vizazi na vizazi.

TUMSIFU MUNGU WETU MKUU

MASOMO YA BIBLIA: Zaburi 104:1-4, 14-25,
27-30, 33

Je! unawashukuru wazazi wako mara kwa mara kwa mambo wanayokufanyia? Je! unamshukuru mama yako kila siku kwa chakula anachokupikia? Je! unamshukuru baba yako kwa nguo ambazo amekununulia? Ni lazima tuwe na tabia ya kusema "asante" kwa wazazi na marafiki zetu kwa mambo yote wanayotufanyia.


Je! unamsifu Mungu mara kwa mara kwa wema wake kwako? Tunamwomba Mungu vitu vingi, lakini mara kwa mara hatumsifu kwa wema na rehema yake kwetu. Ni lazima tumshukuru kila siku kwa baraka zake.

Kitabu cha Zaburi ni kitabu cha sifa. Waebrania walitumia kitabu hiki kama kitabu chao cha nyimbo. Walipoku-mbuka jinsi Mungu aliwatoa katika utumwa nchini Misri, mioyo yao ilijaa shukrani na sifa kwa Mungu. Mambo mengi yaliyowapata wakati Mungu alipowaongoza kutoka Misri yanasimuliwa katika Zaburi.

Kifungu cha kwanza cha Zaburi 104 kinasema, "Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana. Wewe Bwana, Mungu wangu, umejifanya mkuu sana." Kisha, Daudi ambaye ni mwandishi wa Zaburi anazungumza juu ya vitu ambavyo Mungu ameumba. Alipotazama ulimwengu alimsifu Mungu kwa vitu vyote ambavyo ametupa. Hata wanyama Mungu

MUNGU WETU MKUU

amewapa chakula na maji ya kunywa. Jua linaangaza mchana. Mwezi unang'aa usiku na kwa msaada wake tunajua miezi na majira ya mwaka.



"Ee Bwana, jinsi yalivyo mengi mate-
ndo yako! Kwa hekima umevifanya vyote
pia. Dunia imejaa mali zako." (Zaburi
104:24) Daudi alisema kwamba Mungu ali-
umba vitu vingi sana. Vitu hivyo vyote
alivyounda vinaonyesha hekima yake.

Tunamsifu Mungu kwa mpango wake wa
wokovu ambao ni wa ajabu. Tunaweza kuwa
watoto wake kama tukimwamini Yesu, Mwana-
we pekee, aliyekufa kwa ajili yetu. Tuna-
mshukuru kwa kutuonyesha njia inayotuo-
ngoza kwa uzima wa milele.

Tunamsifu Mungu kwa utunzi wake
kwetu kila siku. Tunamsifu kwa msamaha
wake. Yeye ni mvema sana kutupa mahitaji
yetu yote.

Tunamsifu Mungu kwa Biblia, kitabu
chake kitakatifu. Anatawambia habari zake

zote katika Biblia. Anatuonyesha njia ya wokovu. Tunamsifu Mungu kwa Roho Mtakatifu na kuwako kwake katika roho zetu wakati tunapookolewa.

Daudi alisema katika Zaburi 104:33, "Nitamwimbia Bwana maadamu ninaishi; nitamshangilia Mungu wangu nikiwa hai." Alikuwa na furaha na moyo wake ulijaa sifa kwa Mungu. Alisema angemwimbia Bwana maadamu anaishi. Je! unampenda Mungu sana jinsi hiyo? Je! moyo wako unajaa sifa kwa Mungu?

Tunapomjua Mungu kweli na kufahamu mambo ambayo amekwisha kutufanyia sisi pia, tutamsifu maadamu tunaishi.

KAZI YA KUFANYA:

Hapa kuna maswali kutoka Zaburi 104 ambayo ni andiko la somo hili. Uisome kwa uangalifu kabla kuanza kuandika majibu.

1. Mungu amejivika nini? _____
(kifungu cha 1)
2. Ni nini kinachoitwa pazia? _____
(kifungu cha 2)
3. Gari la Mungu ni nini? _____
(kifungu cha 3)
4. Watumishi wa Mungu ni nani? _____
(kifungu cha 4)

MUNGU WETU MKUU

5. Kuna nini katika milima mirefu?
_____ (kifungu cha 18)
6. Mwezi ulifanywa kwa ajili gani?
_____ (kifungu cha 19)
7. Wanyama wa mwitu hutambaa nje
wakati gani? _____ (kif. 20)
8. Mungu huyameesha majani kwa nini?
_____ (kifungu cha 14)
9. Korongo hufanya kitundu chake
wapi? _____ (kifungu cha
17)
10. Mwandishi wa Zaburi alisema ata-
mwimbia Mungu maadamu anafanya
nini? _____ (kifungu cha
33)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana.
Wewe, Bwana, Mungu wangu, umejifa-
nya mkuu sana." Zaburi 104:1*

Tunapofikiria hasa ukuu wa Mungu, tunamsifu Bwana kama Daudi alivyomsifu. Mwanadamu ni kiumbe kidogo sana. Ulimwengu wetu ni mkubwa sana. Daudi alisema katika Zaburi 8:4, "Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na binadamu hata umwanga-
lie?" Lakini Mungu wetu mkuu anatupenda sana na anatutunza. Mwabudu Mungu **sasa**. Labda ungeanza maombi yako kwa maneno haya, "Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana."

MANENO YA KUJIFUNZA:

majira ya mwaka.....wakati wa mwaka.
Majira ya mvua ni
masika, na majira
ya moto ni kianga-
zi.
korongo.....ndege mwenye shi-
ngo ndefu na miguu
mirefu.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Zaburi 104:1-4, 14-25, 27-30, 33

Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA.
Wewe, BWANA, Mungu wangu, Umejifanya
mkuu sana; Umejivika heshima na adhama.
(2) Umejivika nuru kama vazi; Umezita-
ndika mbingu kama pazia; (3) Na kuziweka
nguzo za orofa zake majini. Huyafanya
mawingu kuwa gari lake, Na kwenda juu ya
mabawa ya upepo. (4) Huwafanya malaika
zake kuwa pepo, Na watumishi wake kuwa
moto wa miali.

(14) Huyameesha majani kwa makundi,
Na maboga kwa matumizi ya mwanadamu; Ili
atoe chakula katika nchi, (15) Na divai
imfurahishe mtu moyo wake. Aung'aze uso
wake kwa mafuta, Na mkate umburudishe
mtu moyo wake. (16) Miti ya BWANA nayo
imeshiba, Mierezi ya Lebanoni aliyoipa-
nda. (17) Ndimo ndege wafanyamo vitundu
vyao, Na korongo, misunobari ni nyumba
yake. (18) Milima mirefu ndiko waliko
mbuzi wa mwitu, Na magenge ni kimbilio
la wibari. (19) Aliufanya mwezi kwa
ajili ya nyakati, Jua latambua kuchwa
kwake. (20) Wewe hufanya giza, kukawa

usiku, Ndipo atambaapo kila mnyama wa mwitu. (21) Wana-simba hunguruma wakitaka mawindo, Ili kutafuta chakula chao kwa Mungu. (22) Jua lachomoza, wanakwenda zao, Na kujilaza mapangoni mwao. (23) Mwanadamu atoka kwenda zake kazini, Na kwenye utumishi wake mpaka jioni. (24) Ee BWANA, jinsi yalivyo mengi matendo yako! Kwa hekima umevifanya vyote pia. Dunia imejaa mali zako. (25) Bahari iko kule, kubwa na upana, Ndimo mlimo viendavyo visivyohesabika, Viumbe hai vidogo kwa vikubwa.

(27) Hao wote wanakungoja Wewe, Uwape chakula chao kwa wakati wake. (28) Wewe huwapa, Wao wanakiokota; Wewe waukunjua mkono wako, Wao wanashiba mema; (29) Wewe wauficha uso wako, Wao wanafadhaika; Waliondoa pumzi yao, wanakufa, Na kuyarudia mavumbi yao, (30) Waipeleka roho yako, wanaumbwa, Nawe waufanya upya uso wa nchi.

(33) Nitamwimbia BWANA maadamu ninaishi; Nitamshangilia Mungu wangu nikiwa hai.

Nitamwimbia

Bwana

maadamu

ninaishi;

Nitamshangilia

Mungu wangu

nikiwa hai.

Zaburi 104:33

Wayahudi walitumia kitabu cha Zaburi
kama kitabu cha nyimbo

UJUMBE WA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Yohana 1:1-6; 12-17


Je! ungefanya nini kama Mungu angekwambia uende kuwahubiria watu waovu mno ulimwenguni ya kwamba anawapenda na anataka kuwaokoa? Je! ungeogopa? Ungesema kwamba watu hao ni waovu mno hata hawangesikiliza Neno la Mungu?

Somo hili ni juu ya mtu mmoja ambaye Mungu alimwambia kwenda kuhubiri katika mji uliojaa maovu. Mtu huyo aliitwa Yona. Mji huo uliitwa Ninawi.

Ninawi ulikuwa mji mkuu wa Ashuru. Nchi hii ilikuwa yenye nguvu sana. Watu wake walipigana vita daima na watu wa mataifa mengine. Walikuwa wakatili mno na waovu. Waliabudu sanamu iliyoitwa Ashtorethi.

Siku moja nabii Yona alisikia sauti ya Mungu ikimwambia aondoke aende Ninawi. Ilimpasa kuwaonya watu wa Ninawi kwamba njia zao za uovu zingewaletea uangamizi.

Lakini Yona aliogopa kwenda Ninawi. Alikimbia ili apate kujiepusha na uso wa Bwana. Alikwenda Yafa, mji uliokuwa bandarini, akaona merikebu iliyokuwa ikienda Tarshishi, akapanda kwenda huko. Yona alikata shauri kwenda Tarshishi kwa sababu ilikuwa mbali sana na mji wa Ninawi!



Mara tu merikebu ilipoanza kusafiri, upepo mkubwa ulitokea baharini, kukawa na tufani kubwa hata merikebu ikawa kari-bu kuvunjika. Mabaharia waliogopa, waka-tupa shehena iliyokuwa merikebuni baha-rini ili kupunguza uzito wake.

Yona alikuwa amejilaza merikebuni mle, akapata usingizi. Nahodha alimwe-ndea, akamwuliza, "Una nini, Ewe ulalaye usingizi? amka, ukamwombe Mungu wako; labda Mungu huyo atatukumbuka, tusipo-tee." (Yona 1:6)

Walikuwa wakijaribu kujua ni hatia ya nani iliyowaletea tufani hii. Hatimaye Yona aliwaambia kwamba ilikuwa hatia yake. Alisema, "Mimi ni Mwebrania, nami namcha Bwana, Mungu. Ninakimbia ili nipa-te kujiepusha na uso wake."

Mabaharia waliogopa sana. Walimwu-liza Yona, "Tukutende nini ili bahari itulie?" Yona aliwaambia wamkamate

wamtupe baharini na bahari ingeacha ku chafuka. Walipomtupa baharini, bahari iliacha kuchafuka.

Mungu alimtayarisha samaki mkubwa kummeza Yona. Yona alikaa tumboni mwa samaki yule kwa muda wa siku tatu, mchana na usiku. Alipokuwa tumboni mwa samaki yule alitubu kutotii kwake. Alimwomba Mungu kumsamehe. Siku ya tatu, samaki yule alimtapika Yona pwani (nchi kavu).

Mungu alisema tena na Yona. Alimwambia, "Ondoka, uende Ninawi, mji ule mkubwa, ukaihubiri habari nitakayokuamuru." (Yona 3:2)

Wakati huu Yona alikwenda Ninawi. Alipofika aliwahubiria watu. Aliwaambia kwamba mji huo wao ungeangamizwa baada ya siku arobaini. Walimwamini, wakatubu! Hata mfalme wa Ninawi aliamini ujumbe huo ambao Mungu alimtuma Yona kuwapelekea.

Mungu alipoona kwamba watu wa Ninawi walitubu kweli, alighairi neno lile lake baya alilosema kwamba angeangamiza Ninawi. Jambo hili lilimkasirisha Yona sana. Alimwambia Bwana, "...Nalijua ya kuwa wewe u Mungu mwenye neema, umejaa huruma, si mwepesi wa hasira, u mwingi wa rehema, nawe waghairi mabaya." (Yona 4:2) Alijua kwamba Mungu angewasamehe watu hao wa Ninawi kama wangetubu.

Yona alitoka mjini mle. Aliketi chini aone kwamba mji ule ungekuwaje. Alijifanyia kibanda cha majani kumzuia mwangaza mkali wa jua. Baada ya muda usio mrefu majani yale yalinyauka. Kisha Mungu aliufanya mtango kukua ili kuwa kivuli juu ya Yona. Lakini Mungu aliweka tayari buu, nalo lilitafuna mtango ule. Kisha upepo kutoka mashariki ulianza kuvuma. Jua lilianza kuangaza tena juu ya Yona. Yona alifikiri kwamba ilikuwa heri kufa.

Mungu alisema naye. Alimwuliza, "...Je! unatenda vema kukasirika kwa ajili ya mtango?..." (Yona 4:9). Yona alimjibu kwamba ilikuwa haki kukasirika.

Kisha Mungu alimwambia, "...Wewe umeuhurumia mtango, ambao hukuufanyia kazi, wala kuuotesha; ...na mimi je! haikunipasa kuuhurumia Ninawi, mji ule mkubwa; ambao ndani yake wamo watu zaidi ya mia na ishirini elfu, wasioweza kupambanua katika mkono wao wa kulia na mkono wao wa kushoto?..." (Yona 4:10-11a)

Biblia haitwambii mambo ambayo Yona alifikiri. Bila shaka alisikitika kwa kutojali watu wa Ninawi.

Ujumbe wa Mungu ni kwa kila kabila katika kila nchi ulimwenguni. Mungu anataka ujumbe wake ufahamike mahali pote. Hakuna watu walio waovu zaidi ambao Mungu hawezi kuwaokoa. Mungu anatwambia kuwa mashahidi wake. Je! unakubali kumshuhudia mtu ye yote mahali po pote? Je!

MUNGU WETU MKUU

utawaambia kwamba Mungu anawapenda na alimtuma Yesu kufa kwa ajili ya dhambi zao?

KAZI YA KUFANYA:

Je! unakumbuka somo hili kiasi gani? Hapo chini kuna sentensi zinazokupasa kukamilisha. Maneno ya kujaza katika nafasi hizo yameandikwa chini yao. Chagua neno linalofaa na kuliandika katika nafasi ili kukamilisha sentensi.

1. Mungu alimwambia Yona kwenda _____.
2. Yona alikwenda Yafa, akaona merikebu iliyokuwa ikienda _____.
3. Yona _____ ili ajiepushe na uso wa Mungu.
4. Alipokuwa akisafiri ndani ya merikebu _____ kubwa ilitokea baharini.
5. Mabaharia walimtupa Yona baharini. Mungu alimtayarisha _____ mkubwa kummeza Yona.
6. Yona alikaa ndani ya tumbo la samaki yule mkubwa kwa siku _____, mchana na usiku.
7. Yona _____ alipokuwa tumboni mwa samaki yule.

8. Yona alipofika Ninawi, alihubiri kuwaonya watu kwamba Mungu angea-ngamiza mji wao wa Ninawi baada ya siku _____.
9. Watu wa Ninawi waliposikia ujumbe wa Mungu _____.
10. Kwa sababu walitubu, Mungu _____ mji huo wa Ninawi.

(Ninawi, tatu, Tarshishi, alitubu, alikimbia, arobaini, tufani, walitubu, samaki, hakuangamiza).

Maswali ya Kuzungumza:

Yona alikasirika kwa nini wakati Mungu hakuharibu mji wa Ninawi baada ya watu wake kutubu?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Basi ijulikane kwenu ya kwamba wokovu huu wa Mungu umepelekwa kwa mataifa, nao watasikia!"

Matendo 28:28

Inatupasa kumsifu Mungu kila siku kwa sababu ujumbe wake ni kwa Mataifa! Watu ambao hawakuwa Wayahudi waliitwa Mataifa. Sisi ni watu wa mataifa. Mungu anataka tusikie ujumbe wake na kutubu kama watu wa Ninawi walivyofanya. Anataka tuwaambie kila mtu mahali pote kwamba Yesu ndiye Mwokozi wao.

MUNGU WETU MKUU

MANENO YA KUJIFUNZA:

alighairi.....alibadili nia, aliacha
jambo alilokusudia kufanya.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Yona 1:1-6, 12-17

Basi neno la BWANA lilimjia Yona, mwana wa Amitai, kusema, (2) Ondoka, uende Ninawi, mji ule mkubwa, ukapige kelele juu yake; kwa maana uovu wao ume-panda juu mbele zangu. (3) Lakini Yona akaondoka akimbilie Tarshishi, apate kujiepusha na uso wa BWANA; akatelemka hata Yafa, akaona merikebu inayokwenda Tarshishi; basi, akatoa nauli, akapanda merikebuni, aende pamoja nao Tarshishi, ajiepushe na uso wa BWANA. (4) Lakini BWANA alituma upepo mkuu baharini, ikawa tufani kubwa baharini, hata merikebu ikawa karibu na kuvunjika. (5) Basi wale mabaharia wakaogopa, kila mtu akamwomba mungu wake; nao wakatupa baharini shehe-na iliyokuwa merikebuni, ili kuupunguza uzito wake. Lakini Yona alikuwa ameshuka hata pande za ndani za merikebu; akajilaza, akapata usingizi. (6) Basi nahodha akamwendea, akamwambia, Una nini, Ewe ulalaye usingizi? amka, ukamwombe Mungu wako; labda Mungu huyo atatukumbuka, tusipotee.

(12) Naye akawaambia, Nikamateni, mnitupe baharini; basi bahari itawatulilia; kwa maana najua ya kuwa ni kwa ajili yangu tufani hii imewapata. (13) Lakini wale watu wakavuta makasia kwa

nguvu, ili wapate kurudi pwani, wasiweze; kwa maana bahari ilizidi kuwachafukia sana. (14) Basi wakamlilia BWANA, waka-sema, Twakuomba, Ee BWANA, twakuomba, tusiangamie kwa ajili ya uhai wa mtu huyu, wala usitupatilize kwa ajili ya damu isiyo na hatia; kwa maana wewe, BWANA, umefanya kama ulivyopenda. (15) Basi wakamkamata Yona, wakamtupa bahari-ni, nayo bahari ikaacha kuchafuka. (16) Ndipo wale watu wakamwogopa BWANA mno, wakamtolea BWANA sadaka, na kuweka nadhiri. (17) BWANA akaweka tayari samaki mkubwa ili ammeze Yona, naye Yona akawa ndani ya tumbo la samaki yule muda wa siku tatu, mchana na usiku.

UTII KWA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Danieli 6:1,3,4-10,
13-16, 19-22

Danieli alikuwa mmojawapo wa mashujaa tunaojifunza habari zao katika Agano la Kale. Je! unamfahamu mtu gani leo ambaye ni shujaa? Je! mtu huyo ni shujaa kwa nini? Tunaona katika somo hili saba-bu iliyomfanya Danieli kuwa shujaa.

Wakati Danieli alipokuwa kijana alikamatwa pamoja na vijana wengine watatu wa Kiyahudi, wakapelekwa Babeli. Mfalme wa Babeli aliamuru wafundishwe lugha na desturi za Wakaldayo. Pia, aliamuru walishwe chakula cha mfalme na wanyweshwe divai ya mfalme. Lakini Danieli na marafiki zake hao watatu walikataa kula chakula cha mfalme. Hata mwisho wa mafunzo yao ulipotimia, walionekana kuwa na nguvu na hekima zaidi kuliko vijana wengine wote.

Danieli alichaguliwa kuwa mmojawapo wa washauri wa mfalme. Mungu alimpa pia hekima ya kutafsiri ndoto. Unaweza kusoma hadithi juu ya ndoto ya mfalme Nebukadreza katika sura ya pili ya Kitabu cha Danieli. Wakati Mungu alipomfunulia Danieli maana ya ndoto hiyo, Danieli alimwambia mfalme. Kisha mfalme alimfanya kuwa mkuu. Alimfanya kuwa mtawala juu ya nchi yote ya Babeli.

Baada ya muda usio mrefu, nchi ya Babeli ilipata mfalme mpya aliyeitwa

Dario. Danieli alimtumikia vyema. Dario alifikiria kumweka Danieli juu ya ufalme wake wote. Jambo hili liliwafanya maafisa wengine wote kumwonea Danieli wivu. Wali-jaribu kumpata na hatia. Danieli alikuwa mwaminifu. Hakutenda makosa. Kwa hivyo hawakuweza kumpata na hatia.

Walakini, maafisa hawa walikumbuka kwamba Danieli alikuwa mwaminifu katika ibada yake kwa Mungu. Wao hawakumwabudu Mungu. Walijua kwamba Danieli aliomba mara tatu kila siku, kwa hivyo walifanya mpango.

Mpango waliofanya uliwakataza watu kuomba dua kwa Mungu katika muda wa siku thelathini isipokuwa mfalme. Walimwomba mfalme kutia sahihi mpango huo, mfalme akakubali, akatia sahihi yake.

Kisha maafisa hawa walikwenda nyumbani kwa Danieli, wakamkuta akimwomba Mungu kama ilivyokuwa desturi yake. Danieli alijua sheria ile iliyokataza watu kuomba dua, lakini yeye alikata shauri kumtii Mungu kuliko kuwatii wana-damu. Danieli aliomba mara tatu kila siku. Wakati alipoomba, madirisha ya chumba chake yalikuwa wazi kukabili Yerusalemu.

Maafisa hawa walipomwona akiomba, walikimbia kwenda kwa mfalme. Walimwuliza, "...Je! hukuitia sahihi ile marufuku, ya kwamba kila mtu atakayeomba dua kwa Mungu awaye yote, au kwa mtu awaye yote, katika muda wa siku thelathini, ila



kwako, Ee mfalme, atatupwa katika tundu la simba?..." (Danieli 6:12a)

Mfalme alijibu, "...Neno hili ni kweli, kama ilivyo sheria ya Wamedi na Waajemi isiyoweza kubadilika." (Danieli 6:12b)

Maafisa hawa walisema, "Yule Danieli aomba dua mara tatu kila siku. Anakataa kutii sheria yako."

Mfalme alihuzunika sana. Alimpenda Danieli na alijaribu kufikiria njia ya kumwepusha Danieli adhabu ya sheria ile. Lakini alijua kwamba alikwisha kutia sahihi yake kwa sheria ile. Hangeweza

kuibadili. Hatimaye aliwaamuru watu wake kumkamata Danieli na kumleta mbele yake. Alimwambia Danieli, "Mungu wako unayemtumikia daima, yeye atakuponya." (Danieli 6:16b)

Mfalme hakulala usiku ule wote. Alikataa kula. Kesho yake asubuhi alikwenda haraka mpaka penye tundu la simba. Alimlilia Danieli kwa sauti ya huzuni, akasema, "...Ee Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai, je! Mungu wako, unayemtumikia daima, aweza kukuponya na simba hawa?" (Danieli 6:20b)



Danieli alimjibu, "...Ee mfalme, uishi milele. Mungu wangu amemtuma malaika wake, naye ameyafumba makanwa ya simba, nao hawakunidhuru; kwa kuwa mbele zake mimi nalionekana kuwa sina hatia; tena, mbele yako, Ee mfalme, sikukosa neno." (Danieli 6:21b-22)

MUNGU WETU MKUU

Mfalme alifurahi sana na aliamuru Danieli atolewe katika tundu lile la simba. Kisha alitoa amri kwamba ilimpasa kila mtu aliyekuwa katika utawala wake kutetemeka na kuogopa mbele za Mungu wa Danieli.

Je! umeona sababu iliyomfanya Daudi kuwa shujaa? Alikata shauri moyoni mwake kumtii Mungu hata kama kufanya hivyo kungemletea kifo. Alijua Mungu angemli-nda. Hakuogopa kutenda jambo alilojua kwamba lilikuwa haki.

Je! umepata kutomtii Mungu kwa saba-bu ya kuogopa mambo ambayo marafiki zako watasema? Danieli hakuwaogopa simba wale waliokuwa na njaa! Baadhi yetu wanaogopa kuchekwa kwa ajili ya imani yetu katika Mungu.

Hakuna jambo lililo muhimu zaidi kuliko kuwa mwaminifu kwa Mungu. Ni lazima watoto wa Mungu kutii amri zote anazotupa katika Neno lake. Je! unazungu-mza na Mungu wewe mwenyewe kila siku kama Daudi alivyofanya? Ikiwa huzungumzi naye, chagua wakati maalum wa kuomba peke yako. Mungu anataka umwambie shida zako na umwombe mahitaji yako. Lakini kabla ya kumwomba kitu cho chote, umsifu na umshukuru kwa baraka zake zote kwako.

KAZI YA KUFANYA:

Hapo chini kuna sentensi zinazosi-mulia mambo yaliyofanyika katika somo hili letu la leo. Andika namba 1 katika mstari ulio kando ya jambo lililofanyika

baada ya jambo lile la kwanza. Endelea kufanya hivyo mpaka sentensi zote zimalizike.

- Danieli alimtafsiria mfalme Nebukadreza ndoto yake.
- Maafisa wa mfalme walifanya mpango ili Danieli angeweza kukamatwa na kutupwa katika tundu la simba.
- Danieli alikamatwa mateka akapelekwa Babeli.
- Maafisa wa mfalme walimwona Danieli akiomba.
- Danieli pamoja na marafiki zake watatu walikataa kula chakula cha mfalme.
- Mfalme Dario alimfanya Danieli kuwa mkuu wa maafisa wote. Maafisa hao walimwonea wivu.
- Danieli alitupwa katika tundu la simba.
- Mfalme aliamuru kwamba ilimpasa kila mtu kutetemeka na kuogopa mbele za Mungu wa Danieli.

Maswali ya Kuzungumza:

Tukimwomba Mungu, hatutatupwa katika tundu la simba. Lakini wakati mwingine ni lazima tuwe mashujaa tukitaka kutii amri za Mungu. Zungumza juu ya njia

MUNGU WETU MKUU

nyingine ambazo ni lazima uwe shujaa ili uweze kuwa Mkristo sasa.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Kumcha Bwana ndio mwanzo wa hekima, wote wafanyao hayo wana akili njema, sifa zake zakaa milele."

Zaburi 111:10

Njia nyingine ya kueleza sehemu ya kwanza ya kifungu chetu cha kukumbuka ni kusema watu ni wapumbavu sana kumkataa Mungu! Mungu hutenda jambo analosema. Neno "kumcha" maana yake huheshimu amri za Mungu na kuzitii. Tusipofanya kama Mungu anavyosema, tutakuwa na taabu nyingi sana baadaye. Ukitaka hekima ya kweli, umche Mungu na umfuate.

MANENO YA KUJIFUNZA:

dua.....maombi au sala. Kuomba
dua ni kumwomba Mungu
haja fulani.

kukabili.....kuelekea upande fulani.
tundu.....shimo la wanyama.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Danieli 6:1,3,4-10, 13-16, 19-22

Ilimpendeza Dario kuweka juu ya ufalme maliwali mia na ishirini, wawe juu ya ufalme wote; (3) Basi Danieli huyo alipata sifa kuliko wakubwa na maliwali, kwa kuwa roho bora ilikuwa ndani yake; naye mfalme akaazimu kumweka juu ya ufalme wote.

(4) Basi mawaziri na maamiri waka-
 tafuta sana kupata sababu za kumshitaki
 Danieli kwa habari za mambo ya ufalme;
 lakini hawakuweza kuona sababu wala kosa;
 kwa maana alikuwa mwaminifu, wala haliku-
 onekana kosa wala hatia ndani yake. (5)
 Ndipo wale watu wakasema, Hatutapata
 sababu ya kumshitaki Danieli huyo, tusi-
 poipata katika mambo ya sheria ya Mungu
 wake. (6) Basi wale mawaziri na maamiri
 wakakusanyika pamoja mbele ya mfalme,
 wakamwambia hivi, Mfalme Dario, uishi
 milele. (7) Mawaziri wote wa ufalme, na
 manaibu, na maamiri, na madiwani, na
 maliwali, wamefanya shauri pamoja ili
 kuweka amri ya kifalme; na kupiga marufu-
 ku, ya kwamba mtu ye yote atakayeomba dua
 kwa Mungu awaye yote, au kwa mtu awaye
 yote, katika muda wa siku thelathini,
 ila kwako, Ee mfalme, atatupwa katika
 tundu la simba. (8) Sasa, Ee mfalme,
 piga marufuku, ukatie sahihi maandiko
 haya, yasibadilike, kama ilivyo sheria
 ya Wamedi na Waajemi, isiyoweza kubadi-
 lika. (9) Basi mfalme Dario akayatia
 sahihi maandiko yale, na ile marufuku.

(10) Hata Danieli, alipojua ya kuwa
 yale maandiko yamekwisha kutiwa sahihi,
 akaingia nyumbani mwake; (na madirisha
 katika chumba chake yalikuwa yamefungu-
 liwa kukabili Yerusalemu), akapiga magoti
 mara tatu kila siku, akasali, akashukuru
 mbele za Mungu wake, kama alivyokuwa aki-
 fanya tokea hapo. (13) Basi wakajibu,
 wakasema mbele ya mfalme, Yule Danieli,
 aliye mmoja wa wana wa wale waliohami-
 shwa wa Yuda, hakujali wewe, Ee mfalme,
 wala ile marufuku uliyoitia sahihi, bali




aomba dua mara tatu kila siku. (14) Basi mfalme aliposikia maneno haya alikasirika sana, akakaza moyo wake ili kumponya Danieli; akajitaabisha kumwoko hata jua likachwa. (15) Ndipo watu wale wakakusanyika pamoja mbele ya mfalme, wakamwambia mfalme, Ee mfalme, ujue ya kuwa ni sheria ya Wamedi na Waajemi, lisibadilike neno lo lote lililo marufuku, wala amri yo yote iliyowekwa na mfalme. (16) Basi mfalme akatoa amri, nao wakamleta Danieli, wakamtupa katika tundu la simba. Mfalme akanena, akamwambia Danieli, Mungu wako unayemtumikia daima, yeye atakuponya. (19) Asubuhi mfalme akaondoka mapema, akaenda kwa haraka mpaka penye lile tundu la simba. (20) Naye alipolikaribia lile tundu, akamlilia Danieli kwa sauti ya huzuni; mfalme akanena; akamwambia Danieli, Ee Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai, je! Mungu wako, unayemtumikia daima, aweza kukuponya na simba hawa? (21) Ndipo Danieli akamwambia mfalme, Ee mfalme, uishi milele. (22) Mungu wangu amemtuma malaika wake, naye ameyafumba makanwa ya simba, nao hawakunidhuru; kwa kuwa mbele zake mimi nalionekana kuwa sina hatia; tena mbele yako, Ee mfalme, sikukosa neno.

HUKUMU YA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Amosi 1:1, 2; 7:7-17

Je! unapokataa kuwatii wazazi wako unapatwa na jambo gani? Mwalimu wako shuleni hukufanyia nini wakati unapovunja sheria? Kwa kujibu maswali haya, kwa hakika utasema unaadhibiwa.

Miji na vijiji vyetu vina sheria zao. Sheria hizi zinatusaidia na zinatulinda. Wakati mtu anapovunja sheria, anatozwa pesa au anafungwa gerehani.



Mungu ana sheria zake ambazo ametupa katika Biblia ambayo ni Neno lake. Wakati tunapovunja sheria hizo tunaadhibiwa. Hukumu ya Mungu inawajia wale wanaokataa kufanya kama anavyosema. Lakini Mungu hutuonya juu ya mambo yatakayotupata tukikataa kumtii. Tukisikiliza na kumfuata na kutubu dhambi zetu, ataturehemu na atatusamehe.

Amosi alikuwa nabii wa Mungu. Injili aliyohubiri ni sehemu ya kitabu cha Agano la Kale. Sehemu hiyo inaitwa kitabu cha Amosi.

MUNGU WETU MKUU

Amosi alikuwa mwenyeji wa Tekoa. Mji huu ulikuwa maili sita kusini ya Bethlehemu katika nchi ya milima ya Yuda. Amosi kama manabii wengine wa Mungu, alitumia wakati wake mwingi sana jangwani. Jangwa lilikuwa mahali pazuri sana kumfikiria Mungu na kujifunza habari zake.

Amosi alikuwa mchungaji. Siku moja alipokuwa akichunga kondoo, Mungu alisema naye, akamwambia mambo mengine ambayo yangefanyika kwa nchi ya Israeli.

Kulikuwa na amani Israeli kwa muda wa miaka mingi. Watu wengi walitajirika sana. Walikuwa na nyumba nzuri. Hata wengine walikuwa na nyumba mbili. Walitumia wakati mwingi katika kunywa na kula. Walikuwa na nguo nzuri. Lakini matajiri walipata utajiri wao kwa njia zisizo haki.

Watu wengi walikuwa watumwa na maskini. Matajiri hawakujali maskini. Wauzaji wengi walikuwa wadanganyifu na wakatili kwa maskini. Waamuzi wengi walikuwa wadanganyifu.

Watu walionekana kama wenye dini sana. Walikwenda hekaluni. Walitoa sadaka na dhabihu. Lakini viongozi wa ibada hawakujali vilio vya maskini na watu walihitaji. Walionekana kama walimcha Mungu sana lakini mioyo yao ilikuwa mbali na Mungu.

Tunaambiwa katika Amosi 2:6, "... wamewauza wenye haki kwa fedha, na maskini kwa jozi ya viatu." Haya ndiyo mambo

yaliyofanyika katika nchi yote ya Israeli. Yanaonyesha jinsi Waisraeli walivyo-kuwa wachoyo na wakatili.

Mungu ni mwenye haki na anawakusudia watu wake kuwa watiifu na wenye haki kati yao wenyewe. Mungu hakuruhusu dhambi hizo kuendelea. Alimwambia Amosi kwenda kuwa-ambia watu wa Israeli kwamba wangekamatwa mateka na kupelekwa nchi nyingine.

Wakati Amosi alipoanza kuhubiri, alinena juu ya uovu wa miji na nchi jira-ni za Israeli. Waisraeli walifurahi sana kusikia mambo ambayo yangewapata maadui zao.

Kisha Amosi ali-anza kuhu-biri juu ya dhambi za watu wa Israeli. Aliwaambia kwamba, kwa ajili ya dhambi zao, mfalme wao angeuawa kwa upanga. Wangekama-twa mateka na kupele-kwa nchi nyingine kama wafu-ngwa.



AMOSI AHUBIRI
KATIKA BETHELI

Wakati Amazia, kuhani wa Betheli aliposikia mambo hayo, alimwambia Amosi, "Ewe mwona, nenda zako, ikimbilie nchi ya Yuda, ukale mkate huko, ukatabiri huko; lakini usitabiri tena huku Betheli; kwa maana ni mahali patakatifu pa mfalme, nayo ni nyumba ya kifalme." (Amosi 7:12, 13) Waisraeli hawakutaka kusikia mambo ambayo yangewafanyikia.

Mambo yote ambayo Amosi alitabiri yalifanyika. Miaka sabini baada ya unabii wake, Waisraeli walikamatwa mateka wakapelekwa nchi ya Ashuru. Hukumu ya Mungu iliwajia kama inavyokuja daima kwa watu wanaokataa kumfuata kwa uaminifu na kwa kweli.

Mungu anatwambia wazi kwamba dhambi zetu zitatupata hapana budi. (Soma Hesabu 32:23.) Pia anasema, "Mimi ni Bwana; ndilo jina langu; na utukufu wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa zangu." (Isaya 42:8)

Hakuna kitu tunachoweza kumficha Mungu. Mungu anajua kila kitu. Lakini tunapotubu dhambi zetu wazi kwa Mungu, atatusamehe. Anatupenda sana lakini kwa kuwa yeye ni mwenye haki, ni lazima atuadhibu wakati tunapokataa kumfuata.

Je! kama Yesu angekuja leo angekuta kama hujatubu dhambi yako? Ni lazima tujitayarishe kwa kuja kwake wakati wote kwa sababu hatujui saa atakapokuja tena. Ni lazima tuwe waaminifu kuwashuhudia majirani zetu. Ni lazima tuwaonye juu ya hukumu ya Mungu itakayokuja.

KAZI YA KUFANYA:

Chora mstari kutoka kwa maneno yaliyo kushoto hadi kwa yale yaliyo kulia yanayoyakamilisha.

Walionekana kuwa
watu waliomcha
Mungu lakini
mioyo yao ilikuwa
mbali naye.

uchungaji.

Amosi alikuwa

Amazia.

Amosi alizaliwa
katika mji wa

Tekoa.

Amosi alipoitwa
na Mungu aliku-
wa akifanya kazi
ya

Nabii wa
Mungu.

Kuhani aliyemwa-
mbia Amosi kwe-
nda nyumbani
kwao na kutorudi
kutabiri tena
Betheli aliitwa

Watu wa
Israeli.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Kwa maana imetupasa sisi sote
kudhihirishwa mbele ya kiti cha
hukumu cha Kristo, ili kila mtu
apokee ijara ya mambo aliyotenda
kwa mwili...." 2 Wakorintho 5:10

MUNGU WETU MKUU

Maneno hayo ni wazi. Tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo. Atahukumu maisha yetu. Atahukumu fikira na maneno yetu. Atahukumu mambo tuliyokwisha kufanya. Atahukumu kwa mambo ambayo hatukufanya. Kwa hivyo, tutafuteni ufalme wake kwanza. Mfuateni Yesu kwa uaminifu kila siku. Tiini amri zake. Mtoto mtiifu haogopi cho chote.

MANENO YA KUJIFUNZA:

mwona.....nabii.
mateka.....vitu au watu waliotekwa
vitani.
jozi.....vitu viwili vya namna moja.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Amosi 1:1,2; 7:7-17

Maneno ya Amosi, aliyekuwa mmoja wa wachungaji wa Tekoa; maono aliyoyaona katika habari za Israeli, siku za Uzia, mfalme wa Yuda, na siku za Yeroboamu, mwana wa Yoashi, mfalme wa Israeli, miaka miwili kabla ya tetemeko la nchi. (2) Naye alisema, BWANA atanguruma toka Sayuni, Atatoa sauti yake toka Yerusalem; Na malisho ya wachungaji yataomboleza, Na kilele cha Karmeli kitanyauka.

Amosi 7:7-17

Haya ndiyo aliyonionyesha; na tazama, Bwana alisimama karibu na ukuta uliojengwa kwa timazi, mwenye timazi mkononi mwake. (8) BWANA akaniambia, Amosi, unaona nini? Nikasema, Naona timazi. Ndipo Bwana akasema, Tazama, nitaweka timazi kati ya watu wangu Israeli; sita-

wapita tena kamwe; (9) na mahali palipo-inuka pa Isaka patakuwa ukiwa, na mahali patakatifu pa Israeli pataharibika; nami nitaondoka nishindane na nyumba ya Yero-boamu kwa upanga.

(10) Ndipo Amazia, kuhani wa Betheli, akapeleka habari kwa Yeroboamu, mfalme wa Israeli, akisema, Amosi amefanya fitina juu yako kati ya nyumba ya Israeli; nchi haiwezi kustahimili maneno yake yote. (11) Kwa maana Amosi asema hivi, Yeroboamu atakufa kwa upanga, na bila shaka Israeli atachukuliwa mbali, hali ya kufungwa, atoke katika nchi yake. (12) Tena Amazia akamwambia Amosi, Ewe mwona, nenda zako, ikimbilie nchi ya Yuda, ukale mkate huko, ukatabiri huko; (13) lakini usitabiri tena huku Betheli; kwa maana ni mahali patakatifu pa mfalme, nayo ni nyumba ya kifalme. (14) Ndipo Amosi akajibu akamwambia Amazia, Mimi sikuwa nabii, wala sikuwa mwana wa nabii; bali nalikuwa mchungaji, na mtunza miku-yu; (15) naye BWANA akanitwaa, katika kufuatana na kundi; BWANA akaniambia, Enenda uwatabirie watu wangu Israeli. (16) Basi, sasa lisikie neno la BWANA; Wewe unasema, Usitabiri juu ya Israeli, wala usitoe neno lako juu ya nyumba ya Isaka; (17) kwa hiyo, BWANA asema hivi, Mke wako atakuwa kahaba mjini, na wana wako na binti zako wataanguka kwa upanga, na shamba lako litagawanywa kwa kamba; na wewe mwenyewe utakufa katika nchi iliyo najisi; na bila shaka Israeli atachukuliwa mbali hali ya kufungwa kutoka nchi yake.

MASHARTI YA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Mika 5:10-14; 6:3-8

Ukitaka kazi ya ualimu kuna masharti ambayo ni lazima utimize kwanza kabla Idara ya Ualimu kukuajiri kuwa mwalimu. Ukitaka kuwa mwuguzi, ni lazima kwanza upate mafunzo. Hakuna hospitali inayoweza kukuajiri kama mwuguzi bila mafunzo juu ya kazi hiyo.

Hata Mungu ana masharti kwa watoto wake kutimiza. Mika anatwambia; "Ee mwanaadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema;



MIKA AWAHUBIRIA WANA WA ISRAELI

na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako!" (Mika 6:8) Hili lilikuwa jibu la swali la Mika 6:6 lililouliza: "Nimkaribie Bwana na kitu gani, na kuinama mbele za Mungu aliye juu?"

Katika somo lililopita tulijifunza habari za nabii aliyeitwa Amosi. Mika alikuwa nabii pia, na aliwaonya Waisraeli juu ya hukumu ya Mungu ambayo ingewajia kwa sababu walimwacha. Mungu angeharibu sanamu na miji yao na angewaruhusu maadui zao kuwakamata na kuwahamisha.

Bwana aliwakumbusha jinsi alivyowatoa Misri. Aliwafanya huru kwa sababu walikuwa watumwa. Aliwapa Musa, kiongozi wa ajabu. Aliwaokoa mara kwa mara katika mikono ya maadui zao. Aliwapa chakula na maji.

Mtu mmoja aliuliza, "Nimkaribie Bwana na kitu gani, na kuinama mbele za Mungu aliye juu?" (Mika 6:6) Alitaka kujua kama ilimpasa kuleta sadaka ya kuteketezwa. Je! ilimpasa kuleta elfu za kondoo waume, au elfu kumi za mito ya mafuta? Je! ilimpasa kutoa sadaka ya mzaliwa wake wa kwanza kwa dhambi yake?

Jibu lilikuwa kwamba Bwana anataka tutende haki, tupende rehema, na twende kwa unyenyekevu na Mungu. Mungu hutazama mioyo yetu kabla kutazama mikono yetu! Upendo ni muhimu zaidi kwa Mungu kuliko kazi na vipawa vyetu. Tukimtendea Mungu

MUNGU WETU MKUU

kazi au tukimletea vipawa vyetu bila upendo, itakuwa bure. Sisi pia tutakuwa bure.


Je! "kutenda haki" maana yake ni nini? Maana yake ni kutokuwa na upendeleo na kuwa waaminifu katika ushirikia wetu wote na watu. Ni kumtendea kila mtu mambo sawa bila kujali kabila au nchi anayotoka. Wakati mwingine tunawatendea watu mambo kwa sababu wao ni marafiki zetu.

"Kutenda haki" maana yake ni hatutasema uwongo au maneno matupu juu ya wengine. Maana yake ni tutakuwa waaminifu katika michezo yetu yote. Kwa hakika, maana yake ni hatutadanganya katika kazi yetu shuleni. Tutatii amri za jamii na nchi yetu.

Je! "kupenda rehema" maana yake ni nini? Mungu ni mwenye rehema kwa sababu ana upendo. Ni lazima tuwe wenye rehema kwa sababu tuna upendo. Maana yake ni tutakuwa wavumilivu na wenye kusamehe. Utawatendaje ndugu na dada wanaokuudhi wakati mwingine? Maana yake ni utaonyesha rehema na uvumilivu kwao. Ukiwa na rehema hutakasirika. "Kupenda rehema" maana yake ni kuwa mwenye huruma kwa madui zako. Maana yake ni kuwatendea mema wale wanaokutendea maovu.

Je! unafikiri "kwenda kwa unyenyekevu na Mungu" maana yake ni nini? Tukiwa wanyenyekevu, tunakumbuka kwamba hakuna kitu kinachotupasa kujisifu kwalo. Maana

yake ni tunawafikiria watu wengine kabla ya kujifikiria sisi wenyewe. Tunasoma katika Mithali 16:18 kwamba, "Kiburi hutangulia uangamivu; na roho yenye kutakabari hutangulia maanguko."



Majivuno ni adui mkuu. Je! umepata kuwa na majivuno moyoni mwako kwa sababu wewe ni mchezaji mpira hodari? Labda wewe ni mkimbiaji mzuri. Ni vema kuwa mchezaji mpira hodari au mkimbiaji mzuri, lakini ukumbuke daima kwamba Mungu ndiye amekupa vipawa hivyo. Ukiwa na akili shuleni, ukumbuke kwamba Mungu ndiye amekupa akili. Umsifu Mungu. Watu hawapendi watu wanaojipenda wenyewe!

Kuna vifungu vingi katika Agano Jipya juu ya unyenyekevu. Yesu alisema katika Mathayo 18:4: "Basi, ye yote aji-nyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni."

MUNGU WETU MKUU

Hapa kuna vifungu vingine viwili vya kujifunza juu ya unyenyekevu: "Kwa maana kwa neema niliyopewa namwambia kila mtu aliyeko kwenu asinie makuu kupita ilivyompasa kunia; bali awe na nia ya kiasi, kama Mungu alivyomgawia kila mtu kiasi cha imani." (Warumi 12:3) "Jidhilini mbele za Bwana, naye atawa-kuza." (Yakobo 4:10)

Kwenda kwa unyenyekevu na Mungu maana yake ni kumsifu, kumpenda, kumtii, na kuwa mwaminifu kwake.

Kutenda haki na kupenda rehema maana yake ni kuwa na ushirika halisi na watu. Kwenda kwa unyenyekevu na Mungu ni kuwa na ushirika halisi na Mungu.

Haya ndiyo yaliyokuwa masharti ya Mungu kwa watu wake. Walikuwa bado kutimiza masharti haya. Kwa hivyo, Mungu angewaruhusu maadui zao kuwakamata na kuwahamisha nchi ya mbali.

Wewe je? Unatimiza masharti ya Mungu? Je! ushirika wako na majirani zako na Baba yako aliye mbinguni ni halisi? Je! Mungu akikuonyesha kwamba ushirika wako naye si halisi, au kwamba ushirika wako na watu wengine si halisi, utajariibu kufanya kitu fulani juu ya jambo hilo leo?

KAZI YA KUFANYA:

Vifungu hivi vinatoka katika somo hili. Vikamilishe kwa kuandika maneno

sawa katika nafasi zilizoachwa.

"Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo _____; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda _____, na kupenda _____, na _____ kwa _____ na Mungu wako!"
(Mika 6:8)

"Kwa maana kwa neema niliyopewa namwa-
mbia kila mtu aliyeko kwenu asinie
_____ kupita ilivyompasa kunia;
bali awe na _____ ya _____,
kama Mungu alivyomgawia kila mtu
kiasi cha imani." (Warumi 12:3)

"_____ mbele za Bwana, naye ata-
wakuza." (Yakobo 4:10)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"...Bwana, Mungu wako, anataka nini kwako, ili umche Bwana, Mungu wako, na kwenda katika njia zake zote, na kumpenda, na kumtumikia Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote."
(Kumbukumbu la Torati 10:12)

Andika masharti yote ya Mungu kwa maisha yako ambayo umejifunza leo katika mistari hiyo hapo chini. Utapata masharti mengine katika kifungu cha kukumbuka cha leo.

MASHARTI YA MUNGU KWA MAISHA YANGU

MANENO YA KUJIFUNZA:

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mika 5:10-14; 6:3-8

Kisha itakuwa katika siku hiyo, asema BWANA, nitawakatilia mbali farasi zako watoke kati yako, nami nitayaharibu magari yako ya vita; (11) nami nitaikatilia mbali miji ya nchi yako, na ngome zako zote nitaziangusha; (12) nami nitaikatilia mbali uchawi, usiwe mkononi mwako; wala hutakuwa tena na watu wenye kutabana; (13) nami nitakatilia mbali sanamu zako na nguzo zako, zitoke kati yako; wala hutaiabudu tena kazi ya miko-no yako. (14) Nami nitayang'oa maashera yenu, yasiwe kati yako; nami nitaiangamiza miji yako.

Mika 6:3-8

Enyi watu wangu, nimewatenda nini? nami nimewachosha kwa habari gani? shuhudieni juu yangu. (4) Kwa maana nalikupa-ndisha kutoka nchi ya Misri, na kuukomboa utoke katika nyumba ya utumwa, nami naliwapeleka Musa, na Haruni, na Miriamu, watangulie mbele yako. (5) Enyi watu wangu, kumbukeni sasa alivyouliza Balaki, mfalme wa Moabu, na alivyojibu Balaamu, mwana wa Beori; kumbukeni toka Shitimu hata Gilgali, mpate kuyajua matendo ya haki ya BWANA.

(6) Nimkaribie BWANA na kitu gani, na kuinama mbele za Mungu aliye juu? Je! nimkaribie na sadaka za kuteketezwa, na ndama za umri wa mwaka mmoja? (7) Je! BWANA atapendezwa na elfu za kondoo waume, au na elfu kumi za mito ya mafuta? Je! nimtoe mzaliwa wangu wa kwanza kwa kosa langu, mzao wa mwili wangu kwa dhambi ya roho yangu? (8) Ee mwanadamu, wewe amekuonyesha yaliyo neme? ee BWANA anataka ka nini kwako? ile kutokana na kosa ya nda rehema. na kwanza kuu inyenvekevu na

MUNGU AMWITA NABII

MASOMO YA BIBLIA: Yeremia 1:6-8; 18:3-6

Wakati Mungu anapotuita kumfanyia kazi, tunakuwana hakikisho kwamba atatupa hekima kuifanya kazi hiyo. Tunaweza kuwa wadhaifu, lakini atatupa nguvu. Tunaweza kuogopa, lakini atatupa ushujaa. Tunaweza kufikiri kwamba tu wadogo sana, lakini atatwambia mambo ya kufanya.

Leo tunajifunza habari za nabii Yeremia aliyemhubiria Mungu miaka mingi sana. Alihubiri wakati wa utawala wa wafalme watatu wa Yuda. Wafalme hawa walikuwa Yosia, Yehoyakimu na Zedekia.

Yeremia alizaliwa Anathothi, kijiji kidogo kilichokuwa karibu na Yerusalemu. Hilkia, baba yake, alikuwa kuhani. Bwana alimwita Yeremia, akamwambia, "Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua, na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa; nimekuweka kuwa nabii wa mataifa." (Yeremia 1:5)

Alimjibu Mungu kwamba alikuwa mtoto. Lakini Mungu alimwambia, "...Usiseme, Mimi ni mtoto; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru." (Yeremia 1:7)

Ujumbe wa Mungu ambao Yeremia angehubiri ulisema kwamba nchi ya Yuda ingeangamizwa. Watu wake watakatwa mateka na kuhamishwa. Nchi ya kaskazini iliyoitwa Babeli ndiyo ingeteka nchi yao ya Yuda.

Wakati Mungu alipowaita Waisraeli kuwa watu wake maalum, walimpenda. Walimwabudu na walimtii. Lakini walijaribu uvumilivu wa Mungu kwa muda wa miaka mingi sana. Walitenda dhambi na kutubu mara kwa mara. Sasa walipotea kabisa dhambini. Walikataa kumrudia Mungu. Wakati Yeremia alipojaribu kuwaonya, walikataa kumsikiliza.

Mungu aliwapenda Waisraeli kwa sababu aliwachagua kuwa watu wake maalum. Alitaka wamrudie. Alikwisha kuwapa nafasi nyingi sana kutubu. Kwa sababu Mungu ni mwenye haki hawezi kuvumilia dhambi. Alikata shauri kuwaadhibu Waisraeli.

Siku moja Mungu alimwambia Yeremia kwenda nyumbani kwa mfinyanzi. (Soma Yeremia 18.) Wakati Yeremia alipomtazama



MUNGU WETU MKUU

mfinyanzi, alimwona akichukua chombo alichofinyanga na kukiharibu tena. Hakufurahi nacho kwa sababu kilikuwa na tundu. Alianza kukifanyiza tena kuwa chombo kingine.

Mara moja Yeremia alielewa maana yake. Watu wa Yuda walikuwa kama udongo. Mungu alikuwa mfinyanzi. Angewaharibu kwa sababu walikataa kufuata mpango wake. Angewafanya kuwa wema ili kuweza kumtumikia.

Yeremia alipojaribu kuwaonya watu wa Yerusalemu walikasirika sana na hawakutaka kumsikiliza. Mahubiri mengi ya Yeremia yaliandikwa na mtu mmoja aliyeitwa Baruku katika hati ya kuviringisha. Siku moja Baruku alisoma hati hiyo hekai. Alisoma upendo na onyo la Mungu kwa watu wa Yuda.

Mtu mmoja alisikia maandiko hayo akasema kwamba ilikuwa lazima mfalme pia kuyasikia. Hati ile ilipelekwa kwa mfalme. Kisha mtu mmoja akaanza kumsomea mfalme Yehoyakimu. Mfalme alinyosha mko-no wake, akatwaa hati ile. Alichukua kisu, akaikata vipande vipande, akavitu-pa katika moto uliokuwa karibu naye, vikateketea.

Ilimbidi Yeremia kuanza tena kumwambia Baruku ujumbe aliopewa na Mungu kuan-dika katika hati nyingine mpya. Labda kama ingalikuwa sisi tungalichoka kuan-dika tena ujumbe wa Mungu. Lakini Yeremia hakuchoka. Alihubiri kwa miaka

arobaini na moja. Lakini watu hawakumsi-kiliza kamwe.

Walimwita msaliti. Walimpiga na kumfunga gerezani. Alihuzunika sana kwamba watu hao walikataa kumsikiliza. Alilia mara nyingi wakati alipofikiria uovu wa watu hao na kukataa kwao kumrudia Mungu.

Je! Yeremia alishindwa kutimiza huduma yake? La, alikuwa mwaminifu kwa mwito wa Mungu kwake. Alikuwa mtumishi mwaminifu na alihubiri mambo ambayo Mungu alimwambia kuhubiri. Mambo yote ambayo Mungu alisema kwamba yangefanyika, yalifanyika. Babeli ilishinda Yerusalemu. Hekalu liliteketezwa. Kuta za mji zilibomolewa. Hazina nyingi za hekalu na za makao ya mfalme zilitwaliwa zikapelekwa Babeli. Watu ambao hawakuuawa walikamatwa mateka, wakapelekwa Babeli kama watumwa wa mfalme na wanawe.

Je! uko tayari kuwa mwaminifu kwa mwito wa Mungu katika maisha yako? Je! unakubali kutii Neno la Mungu? Mungu atakuadhibu kama hutii kwa sababu yeye ni Baba mwenye upendo. Anajua mambo yaliyo mema kwako.

Mungu alimtunza Yeremia katika miaka ile arobaini na moja ambayo Yeremia alihubiri. Vivyo hivyo Mungu atatutunza sisi kama tutakuwa waaminifu kwake.

KAZI YA KUFANYA:

Hapa kuna maswali kutoka somo hili la leo. Majibu yao yameandikwa chini yao. Chagua jibu lililosawa na kuliandika katika mstari unaofaa.

1. Yeremia alikuwa mwana wa Hilkia. Hilkia alikuwa _____.
2. Wakati Mungu alipomwita Yeremia, jibu lake kwa Mungu lilikuwa, "Mimi ni _____."
3. Ujumbe wa Mungu ambao Yeremia ali-hubiri katika Yuda ulisema kwamba watu wa Yuda _____.
4. Wangepelekwa kwa nchi ya _____ kama wafungwa.
5. Siku moja Mungu alimwambia Yeremia kwenda kwa nyumba ya _____.
6. Ujumbe wa Mungu ambao Yeremia ali-hubiri uliandikwa katika _____.
7. Wakati mfalme Yehoyakimu aliposo-mewa ujumbe huo, alichukua hati _____, akaitupa _____.

(Majibu: wangekamatwa mateka, mfinyanzi, Baruku, hati ya kuviringisha, motoni, akaikata, mtoto, kuhani, Babeli.)

Maswali ya Kuzungumza:

Yeremia aliitwa msaliti. Alipigwa na alifungwa gereza. Waisraeli hawakumsikiliza. Je! alishindwa kutimiza huduma yake? Toa sababu ya majibu yako.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"...Usiseme, Mimi ni mtoto; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru." Yeremia 1:7

Mungu hana masharti kwa umri unaotupasa kufikia ndipo tuweze kumtumikia. Tunaweza kumtumikia tukiwa na umri wote kama wa miaka kumi, ishirini, au arobaini. Mungu anayo kazi anayokutana wewe kufanya. Atakuongoza kwa watu utakowashuhudia habari za Yesu. Atakusaidia kujua mambo ya kusema. Lakini ni lazima ujifunze Biblia yako ili uweze kujua vifungu utakavyotumia. Roho Mtakatifu hutumia Neno la Mungu kama upanga.

MANENO YA KUJIFUNZA:

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Yeremia 1:6-8; 18:3-6

Ndipo niliposema, Aa, Bwana MUNGU! tazama, siwezi kusema; maana mimi ni mtoto. (7) Lakini BWANA akaniambia,

MUNGU WETU MKUU

Usiseme, Mimi ni mtoto; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru. (8) Usiogope kwa sababu ya hao; maana mimi nipo pamoja nawe nikuokoe, asema BWANA.

18:3-6

Basi nikashuka mpaka nyumba ya mfinyanzi, na tazama, alikuwa akifanya kazi yake kwa magurudumu. (4) Na chombo kile, alichokuwa akikifinyanga, kilipoharibika mkononi mwake yule mfinyanzi, alikifanyiza tena kuwa chombo kingine, kama alivyoona vema yule mfinyanzi kukifanya.

(5) Ndipo neno la BWANA likanijia, kusema, (6) Ee nyumba ya Israeli, je! siwezi mimi kuwatendea ninyi vile vile kama mfinyanzi huyu alivyotenda? asema BWANA, Angalieni, kama udongo ulivyo katika mkono wa mfinyanzi, ndivyo mlivyo ninyi katika mkono wangu, Ee nyumba ya Israeli.

MASIHI ATABIRIWA

MASOMO YA BIBLIA: Isaya 9:1-6; 53:4-6

Tumemaliza kujifunza masomo matano juu ya manabii. Manabii walikuwa mashujaa waliohubiri ujumbe walioambiwa na Mungu kuhubiri. Mojawapo wa ujumbe mkuu wa manabii ulieleza kwamba Mwokozi angekuja ulimwenguni. Ujumbe huo ndilo somo letu la leo.

Nabii Isaya alikuwa mwana wa Amosi na alizaliwa Yerusalemu mwaka wa 760 kabla Kristo kuzaliwa. Alianza kuhubiri mwaka ule ambao Uzia mfalme wa Yuda alipokufa. Alihubiri miaka arobaini kwa wafalme, wana wa mfalme, na watu wote. Alihubiri ujumbe aliopewa na Mungu kwa uaminifu sana.

Isaya, kama manabii wengine tuliokwisha kujifunza habari zao, aliona uovu wa watu. Walikataa kumwabudu Mungu kama Mungu mmoja wa kweli. Alijua kwamba Mungu angewaadhibu watu hao kwa kuwaruhusu maadui zao kuwakamata mateka na kuwahamisha kama wafungwa. Isaya alijua kwamba baada ya watu hao kuwa wafungwa kwa miaka 70, Mungu angewarudisha tena katika nchi yao ya Yuda. Pia, alijua kwamba Mungu angemtuma Mwanawe ulimwenguni kufa kwa ajili ya dhambi za watu wote. Angekuwa Mwokozi ambaye angetukomboza katika dhambi zetu.

Tunasoma katika Isaya 9:6-7; "Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme uta-

kuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuategemeza kwa hukumu na kwa haki; tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo."


Isaya alitabiri katika sura ya 53 kwamba Yesu angedharauliwa na kukataliwa. Angechukua dhambi zetu. (Soma Isaya 53:4-6 sasa.)

Isaya alitabiri kwamba Yesu angezaliwa na bikira. Tunasoma katika Isaya 7:14, "...Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli." Isaya alisema kwamba mtoto Yesu angetoka katika jamaa ya Daudi. (Soma Isaya 11:1.)

Nabii Mika alitabiri kwamba Yesu angezaliwa Bethlehemu. Alisema kwamba ingawa Bethlehemu ulikuwa mji mdogo katika Yuda, Mfalme angezaliwa huko. Mfalme huyo hangekuwa wa kidunia kama wafalme wengine waliokuwa nao kabla kuhamishwa. Angekuwa mfalme ambaye angetawala milele.

Isaya alisema kwamba Yesu angekuwa kama mchungaji. "Tazameni, Bwana Mungu atakuja kama shujaa, na mkono wake ndio utakaomtawalia; tazameni, thawabu yake i pamoja naye, na ijara yake i mbele zake. Atalilisha kundi lake kama mchungaji, atawakusanya wana-kondoo mikononi

mwake; na kuwachukua kifuani mwake, nao wanyonyeshao atawaongoza polepole."
(Isaya 40:10-11)



Tulijifunza juu ya upendo wa Mungu katika somo la pili. Tulisoma kwamba Yesu alizungumza juu yake mwenyewe kama mchungaji. (Soma Yohana 10:11.)

Wakati wa Krismasi tuna mambo mengi ya kumsifu Mungu, lakini wakati huu tuna fikiria kuzaliwa kwa Mwanawe, Yesu ambaye ni Mwokozi wetu.

Fikiria! Isaya alitabiri kuzaliwa kwa Yesu miaka mia saba kabla Yesu kuza-liwa. Sasa karibu miaka elfu mbili imekwisha kupita tangu Yesu alipozaliwa Bethlehemu. Tunafurahi sana kusoma hadi-thi hii katika Biblia. Tuna wajibu na

MUNGU WETU MKUU

nafasi kusimulia hadithi hii kwa watu ambao hawajaisikia.

Je! unasimulia hadithi hii? Je! utajaribu kuishiriki na mtu mwingine wakati wa Krismasi?

KAZI YA KUFANYA:

Baadhi ya sentensi hapo chini ni kweli na mengine si kweli. Andika herufi "K" kando ya sentensi ambayo ni kweli na uandike herufi "M" kando ya sentensi ambayo si kweli.

- ___ 1. Manabii walikuwa mashujaa wali-ohubiri ujumbe walioambiwa na Mungu.
- ___ 2. Isaya alianza kuhubiri katika mwaka ambao Mfalme Ahabu alikufa.
- ___ 3. Isaya aliwaambia watu kwamba Mungu angewaadhibu kwa kuwaruhusu maadui zao kuwakamata na kuwapeleka nchi nyingine kama wafungwa.
- ___ 4. Isaya alizaliwa Yerusalemu mwaka wa sabini na sita kabla Yesu kuzaliwa.
- ___ 5. Isaya alisema katika unabii wake kwamba Yesu angekuwa kama tajiri.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Sisi sote kama kondoo tumepotea;
kila mmoja wetu amegeukia njia yake
mwenyewe; na Bwana ameweka juu yake
maovu yetu sisi sote." Isaya 53:6*

Tulikuwa kama kondoo waliopotea
katika hatari kubwa. Mungu alimtuma Mwa-
nawe Yesu kuwa mchungaji wetu. Yesu haku-
tenda dhambi lakini Mungu alimwekea dha-
mbi yako na dhambi za ulimwengu wote.
Upendo wa Mungu ni wa ajabu!

MANENO YA KUJIFUNZA:

(ma)shujaa.....mtu hodari, asiye na
hofu, jasiri.

(ku)tabiri.....kubashiri, kusema haba-
ri za mambo yatakayoku-
ja.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Isaya 9:1-6; 53:4-6

Lakini yeye aliyekuwa katika dhiki
hatakosa changamko. Hapo kwanza aliiingi-
za nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali
katika hali ya kudharauliwa, lakini zama-
ni za mwisho ameifanya kuwa tukufu, kari-
bu na njia ya bahari; ng'ambo ya Yordani,
Galilaya ya mataifa. (2) Watu wale wali-
okwenda katika giza Wameona nuru kuu;
Wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa
mauti, Nuru imewaangaza. (3) Umeliongeza
taifa, umezidisha furaha yao; Wanafurahi
mbele zako, Kama furaha ya wakati wa
mavuno, Kama watu wafurahivyo wagawanyapo

nyara. (4) Kwa maana umeivunja nira ya mzigo wake, na gongo la bega lake, na fimbo yake yeye aliyemwonea, kama katika siku ya Midiani. (5) Maana silaha zote za mtu mwenye silaha wakati wa mshindo, na mavazi yaliyofingirishwa katika damu, yatakuwa tayari kuteketezwa, yatakuwa kuni za kutiwa motoni. (6) Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani.

Isaya 53:4-6

Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. (5) Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. (6) Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.

KRISTO AMEZALIWA

MASOMO YA BIBLIA: Luka 2:1-20

Nchi Ndogo ya Uyahudi (Palestine) ulitawaliwa na mfalme mwenye choyo aliyeitwa Kaisari Augusto. Siku moja alikata shauri kujua idadi ya Wayahudi waliokaa Uyahudi ili wangeweza kumtolea ushuru.

Alitoa amri kwamba watu wote wahesabiwe. Aliamuru kila mtu kwenda kuandikwa jina mjini kwao ambako wazazi wake walikaa. Iliwabidi watu wengine kusafiri mbali.

Kulikuwa na seremala mmoja aliyeitwa Yusufu katika mji mdogo wa Nazareti. Mke wake aliitwa Mariamu. Wote wawili walikwisha kuambiwa na malaika mambo ya kushangaza.

Malaika wa Bwana alimtokea Mariamu usiku mmoja, akamwambia jinsi alivyobairikiwa. Alimwambia kwamba angezaa mtoto mwanamume. Angemwita Yesu. Lakini Mariamu hakujua jinsi mambo hayo yangefanyika kwa sababu hakuwa na mume.

Lakini malaika alimwambia, "Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu."
(Luka 1:35)

Malaika alimtokea Yusufu pia katika ndoto. Alimwambia Yusufu asiogope kumchu-

MUNGU WETU MKUU

kua Mariamu kuwa mke wake. Alisema,
"...mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mta-
katifu. Naye atazaa mwana, nawe utamwita
jina lake Yesu, maana, yeye ndiye ataka-
yewaokoa watu wake na dhambi zao."
(Mathayo 1:20b-21)

Wakati wa Mariamu kuzaa mtoto sasa
ulikaribia. Lakini iliwabidi kwenda
Bethlehemu kuandikisha majina yao na
kulipa ushuru. Ilikuwa lazima kwa kila
mtu kutii amri ya Mfalme Kaisari.

Ilikuwa mwendo wa maili 70 kwenda
Bethlehemu. Mariamu alichoka sana wakati
walipowasili huko. Yusufu alijaribu kuta-
futa nafasi katika nyumba za wageni laki-
ni nyumba hizo zilijaa. Mwisho wake, mtu
mmoja mwenye nyumba ya wageni aliwaambia
kwenda kulala katika zizi.



Usiku huo
Mariamu alimzaa
mtoto Yesu. Ali-
mvika nguo za
kitoto, akamlaza
katika hori ya
kulia ng'ombe.

Usiku huo
pia walikuwako
wachungaji mako-
ndeni wakilinda
kundi lao la
kondoo kwa zamu.
Malaika wa Bwana
aliwatokea kwa

ghafula. Utukufu wa Bwana uliwang'aria
pande zote. Waliogopa sana.

Malaika huyo aliwaambia, "Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaleteta habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana." (Luka 2:10b, 11)

Jeshi
kuu la
mbinguni
walianza
kuimba,
"Atukuzwe
Mungu juu
mbinguni,
na duniani
iwe amani
kwa watu
aliowari-
dhia."
(Luka 2:14)



Wachungaji walijiharakisha kwenda Yerusalemu. Walipofika waliwakuta Mariamu, na Yusufu, na mtoto Yesu aki-lala katika hori.

Masihi ambaye manabii walisema kwa- mba angekuja, sasa alikuja kweli! Wachu- ngaji walimwona kwa macho yao. Walirudi kwa kundi lao la kondoo wakimshukuru na kumsifu Mungu. Walimwambia kila mtu waliyekutana naye habari njema iliyosema, "Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana." (Luka 2:11)

MUNGU WETU MKUU

Je! umekwisha kumkaribisha Yesu moyoni mwako kuwa Mwokozi wako? Ikiwa umekwisha kumkaribisha, je! unamwambia kila mtu habari njema ya wokovu unaojua?

KAZI YA KUFANYA:

Hapa kuna maswali tisa. Jibu la kila swali linapatikana katika kifungu cha kukumbuka kilichoandikwa katika mwisho wa swali. Andika majibu katika mistari iliyo kando ya maswali hayo.

- _____ 1. Malaika alimwambia kuhani mmoja ya kwamba Elisabeti, mke wake, angezaa mtoto mwanamume. Je! kuhani huyo alikuwa nani? (Luka 1:18)
- _____ 2. Je! mtoto wa Mariamu aliitwa nani? (Mathayo 1:21)
- _____ 3. Watu gani waliotoka mashariki wakimtafuta Yesu? (Mathayo 2:1)
- _____ 4. Je! ni kitu gani kilichowangoza watu hao katika safari yao? (Mathayo 2:9)
- _____ 5. Malaika aliyemwambia Mariamu kwamba angezaa mtoto mwanamume aliitwaje? (Luka 1:26)
- _____ 6. Mamaye Yesu aliitwaje? (Mathayo 2:11)

- _____ 7. Je! malaika waliwaambia
watu gani habari za kuzaliwa
kwa Yesu? (Luka 2:8-11)
- _____ 8. Mji ule ambao Yesu alizaliwa
uliitwaje? (Mathayo 2:1)
- _____ 9. Baba mlezi wa Yesu alikuwa
nani? (Mathayo 2:13)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Akamzaa mwanawe, kifungua mimba,
akamvika nguo za kitoto, akamlaza
katika hori ya kulia ng'ombe, kwa
sababu hawakupata nafasi katika
nyumba ya wageni."* Luka 2:7

Mwana pekee wa Mungu alizaliwa kati-
ka zizi. Alizaliwa kama maskini. Kuzaliwa
kwake kulifanyika kama manabii walivyota-
biri. Ni jambo la kuhuzunisha kuona kwa-
mba watu wengi bado hawapendi kumpokea
Yesu maishani mwao. Onyesha upendo wa
Yesu maishani mwako wakati huu wa Krisma-
si. Labda kwa upendo huo utamsaidia mtu
mwingine kumpokea Yesu maishani mwake.

MANENO YA KUJIFUNZA:

konde (makonde).....shamba.
zamu.....muda wa kazi, mche-
zo, tendo, n.k.
zamu ya askari.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Luka 2:1-20

Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu wote wa ulimwengu. (2) Orodha hii ndiyo ya kwanza iliyoandikwa hapo Kirenio alipokuwa liwali wa Shamu. (3) Watu wote wakaenda kuandikwa, kila mtu mjini kwao. (4) Yusufu naye aliondoka Galilaya, toka mji wa Nazareti, akapanda kwenda Uyahudi mpaka mji wa Daudi, uitwao Bethlehemu, kwa kuwa yeye ni wa mbari na jamaa ya Daudi; (5) ili aandikwe pamoja na Mariamu mkewe, ambaye amemposa, naye ana mimba. (6) Ikawa, katika kukaa huko, siku zake za kuzaa zikatimia, (7) akamzaa mwanawe, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.

(8) Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kuli-nda kundi lao kwa zamu usiku. (9) Malaika wa Bwana akawatokea ghafula, utukufu wa Bwana akawang'aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu. (10) Malaika akawaambia, Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletetea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; (11) maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. (12) Na hii ndiyo ishara kwenu; mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe. (13) Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema, (14) Atukuzwe Mungu juu mbinguni,

Na duniani iwe amani kwa watu aliowari-dhia. (15) Ikawa, malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji waliambiana, Haya, na twendeni mpaka Bethlehemu, tukalionne hilo lililofanyika, aliotujulisha Bwana. (16) Wakaenda kwa haraka wakamkuta Mariamu na Yusufu, na yule mtoto mchanga amelala horini. (17) Walipomwona wakatoa habari waliyoambiwa juu ya huyo mtoto. (18) Wote waliosikia wakastaajabu kwa hayo waliyoambiwa na wachungaji. (19) Lakini Mariamu akayaweka maneno hayo yote, akiyafikiri moyoni mwake. (20) Wale wachungaji wakarudi, huku wanamtukuza Mungu na kumsifu kwa mambo yote waliyosikia na kuyaona, kama walivyoambiwa.

TUNU ZETU KWA YESU

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 2:1-12

Tulipojifunza masomo juu ya manabii, tuliona kwamba walitabiri ya kuwa Yesu angekuja ulimwenguni. Angekuwa Mwokozi wa watu wote mahali pote. Ujumbe huo wa manabii juu ya Mwokozi ulienea katika nchi zilizokuwa mbali na Uyahudi (Palestine).

Usiku mmoja wakati kundi la mamajusi mashariki walipokuwa wakijifunza juu ya nyota, waliona kwa ghafula nyota moja iliyong'aa sana upande wa magharibu. Lakini walijua kwamba nyota hiyo ilikuwa ishara kwamba mfalme mpya alizaliwa.

Walijitayarisha kusafiri mbali ili kumwona mfalme huyo mpya. Walichagua tunu nzuri zilizostahili kutolea mfalme, wakazibeba.

Baada ya kusafiri siku nyingi, waliwasili Yerusalemu. Walimwuliza kila mtu waliyekutana naye kuwaonyesha mahali ambapo mfalme mpya alizaliwa. Walisema kwamba waliona nyota yake, na walikuja kumwabudu. Mfalme Herode aliposikia maneno hayo alifadhaika sana. Alituma ujumbe kwa mamajusi hao kuja kwake.

Mamajusi hao walipokuja kwake, alipata kwao hakika ya muda tangu nyota ile ilipoonekana. Kisha aliwaambia, "Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili

mimi nami niende nimsujudie." (Mathayo 2:8)



Mamajusi hao walishika njia, waka-enda Yerusalemu. Waliona nyota ile tena ikisimama juu ya nyumba moja Yerusalemu ambapo mtoto alikuwapo. Walifurahi sana. Waliingia nyumbani humo, wakapiga magoti mbele ya mtoto Yesu, wakamsujudia. Wali-mtolea tunu walizomletea. Tunu hizo zili-kuwa dhahabu, uvumba, na manemane. Kwa kumtolea Yesu tunu hizo, walionyesha upendo wao kwa Mwana wa Mungu.

Wakati wa kurudi kwao, mamajusi hao hawakupitia Yerusalemu. Mungu aliwaonya katika ndoto kurudi kwao kwa njia nyi-ngine.

Yesu alijua kwamba tungetaka kumto-lea tunu zetu. Alisema kwamba tulipomsa-idia mtu mwingine, tulimtolea yeye tunu zetu. (Soma Mathayo 25:40.) Alitoa uhai

MUNGU WETU MKUU

wake msalabani ili wewe na mimi tupate
maima wa milele. Hiyo ndiyo iliyokuwa
tunu yake nzuri sana kwetu. Je! tunaweza
kumtolea Bwana tunu zetu nzuri sana kwa
jinsi gani? Kwa kupokea tunu yake. Je!
utamtolea tunu ya moyo na maisha yako
wakati huu wa Krismasi?

KAZI YA KUFANYA:

Soma sentensi zifuatazo juu ya tunu.
Weka alama hii (✓) katika mstari ulio
kando ya sentensi inayozungumza juu ya
tunu unayofikiri kwamba ilimpendeza Yesu.

— Mariamu alipaka nywele za Yesu
kwa mafuta ya manukato.

— Wafalme wengine walimletea mtoto
Yesu tunu zenye thamani kubwa.

— Mwanamke mmoja maskini alitia
sadaka yake ndogo katika sanduku
la sadaka lililokuwa karibu na
mahali Yesu aliposimama.

— Mtu mmoja alileta pesa zake nyi-
ngi hadharani kabla kuzitia kati-
ka sanduku la sadaka.

— Msichana mmoja mdogo aliweka pesa
zake za kununulia chakula cha
mchana kila siku kwa ajili ya
matoleo ya sadaka ya Shule ya
Jumapili.

— Mchungaji mmoja alimletea mtoto
Yesu mwana-kondoo.

— Mtu mmoja alimruhusu Yesu kuchukua mwana-punda wake kupanda wakati wa kuingia mjini.

— Kijana mmoja alimpa Yesu chakula chake cha mchana.

— Msichana mmoja mdogo alikubali kumpa mwanafunzi mwingine kofia. Lakini kabla ya kumpa, alingojea mpaka wanafunzi wote walipofika darasani kwa sababu alitaka kusi-fiwa.

Ikiwa tunu nyingine hazikumpendeza Yesu, ueleze ni kwa sababu gani hazikumpendeza.



KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Mpeni Bwana utukufu wa jina lake;
leteni sadaka, mje mbele zake...."
1 Mambo ya Nyakati 16:29a

MUNGU WETU MKUU

Mtukuze Bwana kwa kuzungumza juu ya ukuu wake kwa marafiki zako. Weka pesa zako akiba ili uweze kumtolea Mungu fungu lako la kumi na sadaka. Fungu la kumi ni la Mungu. Usipomtolea Mungu fungu la kumi, jua kwamba hujamtolea tunu yo yote.

MANENO YA KUJIFUNZA:

- tunu.....kitu cha thamani, zawa-di.
manukato.....maji au unga unaonukia vizuri, hutumika kufukizia au kunyunizia watu, au nguo kama marashi.
uvumba.....namna ya gundi inayonukia, hutumika kufukizia kama ubani.
manemane.....namna ya utomvu wa miti fulani ulioganda kama sandarusi; hutumikia kufukizia kama ubani.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mathayo 2:1-12


Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalemu, wakisema, (2) Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia. (3) Basi mfalme Herode aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye. (4) Akakusanya wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu, akatafuta habari kwao, Kristo

TUNU ZETU KWA YESU


azaliwa wapi? (5) Nao wakamwambia, Katika Bethlehemu ya Uyahudi; kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii,


(6) Nawe Bethелеhemu, katika nchi ya Yuda, Hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda; Kwa kuwa kwako atatoka mtawala Atakayewachunga watu wangu Israeli.

(7) Kisha Herode akawaita wale mama-jusi faraghani, akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota. (8) Akawapeleka Bethlehemu, akasema, Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie. (9) Nao waliposikia maneno ya mfalme, walishika njia; na tazama, ile nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto. (10) Nao walipoiona ile nyota, wali-furahi furaha kubwa mno. (11) Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia; nao walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu na uvumba na manemane. (12) Nao wakiisha kuonywa na Mungu katika ndoto wasimrudie Herode, wakaenda zao kwao kwa njia nyingine.



Andika katika hati hii va kuvingirisha
mojawapo ya Vifungu vya Kukumbuka vya
mfulizo wa masomo haya ya miezi mitatu
ambacho unakipenda zaidi







BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE

AN AGENCY OF THE BAPTIST MISSION OF EAST AFRICA
TELEPHONE 5424 • P. O. BOX 30370 • NAIROBI, KENYA

